# Nipashe

Jumamosi Juni 8, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579939

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mwalimu shule sekondari afariki kwa kunywa gongo

UKURASA 4




UKURASA 13

# PM aeleza maofisa wa TRA walivyodai rushwa

**ATOBOA** walivyomng'ang'ania mfanyabiashara awape 'kitu kidogo', Rais aagiza washtakiwe, mawaziri watatu wadaiwa kikwazo cha biashara... *Endelea uk. 2 & 3*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**SABABU KUSITISHWA BANDARI B'MOYO HIZI**

RAIS John Magufuli amesema sababu kubwa ya kusitishwa kwa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ni masharti mabovu yaliyopo katika mkataba wa ujenzi wa bandari hiyo...

**UKURASA WA 7**

**WATALII MILIONI 1.4 KUJA NCHINI**

IDADI ya watalii watakaoingia nchini kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 inatarajia kuongezeka kutoka milioni 1.3 hadi ...


## Mwanafunzi kidato cha nne alivyojinusuru kuozwa na baba

UKURASA 4



## JPM afichua mbinu za ukwepaji wa kodi

UKURASA 2

Rais John Magufuli, akizungumza na wafanyabiashara wakubwa kutoka wilaya zote nchini pamoja na wajumbe wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC), Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**


**MICHEZO** AJIBU, MKUDE WAACHWA STARS UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## Mwongozo maduka ya fedha waandaliwa

**Na Gwamaka Alipipi**

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, amesema wanaandaa mwongozo kwa wamiliki wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni (Bureau de Change) ambao utaonesha namna ya kufanya biashara hiyo.

Amesema tangu kufungwa kwa maduka hayo, benki nchini zimekuwa zikikusanya Dola za Marekani milioni 10 kwa siku.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam kwenye mkutano ukiomkutanisha Rais John Magufuli na wawakilishi wa wafanyabiashara kutoka wilaya zote nchini.

"Kwa muda wa wiki tatu sasa benki zetu hazijaja kuchukua fedha za kigeni BoT, bali BoT ndiyo inayokwenda kuchukua fedha hizo kwenye benki," alisema Prof. Luoga.

Alisema kwa sasa BoT inahitaji kuwa na benki zinazopanuka na kuwafikia wananchi, hususan wanaoishi vijijini, pia ziwe na umuhimu kwa wananchi.

Alisema benki nchini zinapaswa kuboreshwa, hivyo BoT itaanza kuwatambua wafanyakazi wa kwenye benki kwa kuwapa ithibati, lengo kuu likiwa ni kuwa na wafanyakazi wenye weledi wa masuala la benki.

Alisema kuteteleka kwa mabenki nchini ni kuteteleka kwa uchumi wa nchi, hivyo BoT itakuwa macho katika kudhibiti benki zote nchini.

Prof. Luoga alisema ukopeshaji wa benki kwa sekta binafsi nchini kwa sasa umefikia asilimia 12.

Akizungumzia suala la kufungwa kwa maduka ya kubadilishia fedha za kigeni, Rais Magufuli alisema kulikuwa na biashara chafu zilizokuwa zinafanywa na baadhi ya wafanyabiashara, wakiwa na lengo la kukwepa kodi.

Alisema kulikuwa na wafanyabiashara waliokuwa wananunua bidhaa nje ya nchi ambapo fedha walikuwa wakisafirisha kwa kutumia maduka hayo.

"Utakuta mtu anakwenda China kununua mzigo, akishanunua mzigo wake anakwenda kwenye duka la kubadilishia fedha za kigeni ambalo lina tawi Tanzania, anawasiliana na ndugu yake aliyeko Tanzania anapeleka fedha hapo," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema serikali itaendelea kuwa macho katika kuyaangalia maduka ya kubadilishia fedha za kigeni wakati wote.

## MKUTANO WA JPM NA WAFA

# Watumishi wa TRA ku

**Romana Mallya**

MAELEZO yaliyotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kuhusu watumishi watatu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhusika katika tukio la kumnyang'anya mfanyabiashara bidhaa zake kwa muda wa miaka mitatu, yalimfanya Rais Magufuli kuagiza wakamatwe na kushtakiwa.

Mbali na kuwakamata na kuwafikisha mahakamani, Rais Magufuli pia aliiagiza Mamlaka hiyo iwasimamishe kazi.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana Ikulu katika mkutano kati yake na wafanyabiashara baada ya Waziri Mkuu kueleza kisa cha mfanyabiashara huyo ambaye mizigo yake ilishikiliwa na TRA kwa muda wa miaka mitatu baada ya kukataa kutoa rushwa ya Sh. milioni



Sehemu ya wafanyabiashara wakubwa kutoka wilaya zote nchini, wakiwa katika Kikao na Rais John Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# JPM afichua mbinu za ukwepaji kodi

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amefichua mbinu zinazotumiwa na wafanyabiashara kukwepa kulipa kodi serikalini, mojawapo ikiwa ni kutengeneza vitabu viwili vya mahesabu kimoja kikiwa na takwimu za uongo na kingine cha ukweli.

Aliyasema hayo kwenye mkutano uliofanyika jana Ikulu jijini Dar es Salaam ambapo Rais Magufuli alikutana na wawakilishi wa wafanyabiashara kutoka wilaya zote nchini na wajumbe wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC).

Akizungumza kwenye mkutano huo, Rais Magufuli alisema kuna wafanyabiashara ambao wanatengeneza vitabu zaidi ya kimoja ili kukwepa kupeleka kodi kubwa ya Ongezeko la Thamani (VAT) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Rais Magufuli alisema linapofika suala la kulipa kodi ya VAT ambayo ni asilimia 18 wengi wamekuwa wakibaki nayo kama mtaji badala ya kuipeleka serikalini, pamoja na kutengeneza vitabu tofauti vya mahesabu.

"Wafanyabiashara wanatengeneza vitabu viwili, kimoja ni cha benki ambacho ndicho chenye mahesabu ya kweli yenye faida, na kingine ni cha TRA, kile kinachopelekwa benki ndicho halisi, lakini kinachopelekwa TRA kinakuwa kimeonesha hasara," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema kuna kampuni fulani mbayo mwaka 2017 taarifa ya benki ilionesha ilipata faida ya Sh. milioni 958, lakini kitabu kilichoenda TRA kilionesha kimepata faida ya Sh. milioni 20.

Rais Magufuli alisema pia kuna kampuni hewa 17,446 nchini ambazo zimesajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), lakini kiuhalisia hazipo wala hazijulikani zilipo, lakini zinakwenda kudai kurejeshewa VAT.

Alisema kuna wafanyabiashara wengine wamekuwa wakikwepa kodi kwa kutoa rushwa na wengine kufanya udalali na kujihusisha na uhalifu.

Pia, alisema wafanyabiashara wengi wamekuwa wakidai marejesho ya fedha ya VAT wakati mauzo yaliyofanyika ni hewa.

"Utakuta mfanyabiashara amenunua mashine kwa Sh. milioni tano, lakini anasema ni Sh. milioni 50, lengo lake apate VAT refund kubwa," alisema Rais Magufuli.

Alisema pia wafanyabiashara wakubwa wamekuwa wakiwaumiza wafanyabiashara wenzao wadogo na wakati kwa kuingiza bidhaa sokoni ambazo hazijalipiwa kodi na kuziuza kwa bei ndogo.

Aliongeza kuwa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) haina mchango wowote kwa wafanyabiashara wanaotoka mkoani.

Hata hivyo, Rais Magufuli alizungumzia changamoto zilizopo upande wa serikali zinazowakwamisha wafanyabiashara nchini.

Rais Magufuli alisema kuna utitiri wa taasisi za udhibiti kama vile Osha, Nemc, TBS, TFDA ambazo zote zimekuwa zikihusika katika kuwalipisha tozo wafanyabiashara.

"Hizo zote zimekuwa ni kikwazo cha kukuza biashara nchini, pia zimekuwa ni chanzo cha kukwamisha biashara Tanzania," alisema Rais Magufuli.

Alisema kuna utitiri wa tozo, ushuru, ada na kodi zinazotozwa na serikali kwa wafanyabiashara, na kwamba kuna kukithiri kwa rushwa kwa baadhi ya taasisi kama bandarini, TRA eneo la mipakani.

Alisema pia hakuna mikakati madhubuti ya kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo na wakati.

"Asilimia 90 ya shughuli za kiuchumi duniani zinafanywa na wajasiriamali wadogo na kati, lakini hapa kwetu hakuna mikakati ya kuwaendeleza, Tumeanzisha EPZD pamoja na TIC kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wakubwa lakini tumeshindwa kuwakumbuka wadogo, na ndiyo sababu nikaamua kutengeneza vitambulisho," alisema Rais Magufuli.

Alisema pia kuna ukosefu wa mitaji ya kuendeshea biashara, ambapo taasisi nyingi za benki zimekuwa zikiweka masharti makubwa, pamoja na riba kubwa huku nyingi zikiwa mjini, hali inayosababisha wengi kutonufaika.

Alisema pia mawakala wa TBS walioko nje ya nchi siyo waaminifu.

## ANYABIASHARA IKULU, DAR

# shtakiwa kwa rushwa

mbili.

Baada ya maelezo ya Majaliwa, Rais Magufuli aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) iwakamate na kuwaweka ndani na wakati kesi hiyo ikiendelea mahakamani, na TRA iwasimamishe kazi.

Kamishna Mkuu wa TRA, Charles Kichere, alikiri kuwa mzigo huo ulikamatwa mwaka 2015 na kushikiliwa kwa muda wa miaka mitatu na ulikabidhiwa juzi kwa mfanyabiashara huyo.

Kichere alisema baada ya tukio hilo Majaliwa alimuita kijana aliyehusika.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli alimtaka Kamishna Kichere ataje jina la kijana huyo ndipo alipojibiwa kuwa,"Mheshimiwa Rais jina la huyu kijana nimelisahau, lakini napenda kukuahidi kuwa nitakupatia."

INAENDELEA UK. 8



# Mawaziri watatu wachongewa kwa Rais

**Na Gwamaka Alipipi**

MAWAZIRI watatu jana walijikuta kwenye wakati mgumu baada ya wafanyabiashara kuwachongea kwa Rais John Magufuli kwamba wameshindwa kutatua kero zilizopo katika sekta zao.

Mawaziri hao ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga.

Wakizungumza mbele ya Rais Magufuli, wafanyabiashara hao 'waliwalipua' mawaziri hao kwa kueleza kwenye wizara zao kuna sheria ambazo zimekuwa zikiwanyonya wakati wakinunua, wakisafirisha bidhaa zao kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Crisant Mzindakaya ambaye ni mkulima anayemiliki kiwanda cha nyama, alisema Tanzania bado kuna hujuma na urasimu hususan katika wizara ya kilimo, kwa kuwa amekuwa akipiga simu na kuandika barua lakini amekuwa hapati mrejesho wowote.

"Nimewahi kuwa mbunge kwa miaka mingi, wizara ambayo inaiangusha Tanzania ni kilimo, Taasisi zote za kilimo zimekufa, mfano Taasisi ya Kilimo Uyole," alisema Mzindakaya. Alisema ununuzi wa mahindi katika mikoa ya Mbeya na Rukwa ni siasa tupu, kwa sababu hakuna bei elekezi ya ununuzi wa zao hilo.

Alisema ni jambo la aibu hadi sasa Tanzania kuendelea kuagiza vyungu pamoja na maua kutoka nje ya nchi, wakati kuna Watanzania wanaweza kufinyanga vyungu vizuri.

"Fedha za kigeni zitumike vizuri, tuache kutumia vibaya, tuna maua mazuri kutoka Arusha, lakini bado tunaagiza nje ya nchi," aliema Mzindakaya.

Francis Noni, mfanyabiashara kutoka mkoa wa Tabora, alisema kilimo bado kipo chini, watumishi wa Mamlaka wa Mapato Tanzania (TRA) wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea ambapo wengi wao wamekuwa wakiwabambikizia kodi kubwa wafanyabiashara.

Emmanuel Soko, mwekezaji kwenye sekta ya elimu na afya, alisema TRA wamekuwa wakikadiria kodi kwa kukisia, ushuru wa huduma umekuwa ukitozwa ovyo. "Ukadiriaji wa kodi siyo rafiki, mwaka jana nilitozwa Sh. 100,00 mwaka huu wananitoza Sh. 200,000 biashara hiyo hiyo," alisema Soko.

Naye Giritu Madura kutoka Shinyanga, alisema ushuru wa huduma unaotozwa na halmashauri imekuwa ikitozwa kwa kuangalia mauzo kuliko faida aliyopata mfanyabiashara.

Henry Mchunga, mfanyabiashara wa mazao mchanganyiko kutoka Simiyu, alisema ubora wa mahindi uko chini kulinganisha na nchi zingine.

Alisema wafanyabiashara wadogo wanaoanza biashara wamekuwa wakifanyiwa makadirio makubwa, hivyo alipendekeza kuwe na muda wa miezi sita kwa TRA kuanza kumkadiria mfanyabiashara mpya, sambamba na VAT kupungua hadi asilimia 16.

INAENDELEA UK. 8

# Rais ataja sababu kusitisha ujenzi bandari ya Bagamoyo

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli amesema sababu kubwa ya kusitishwa kwa ujenzi wa bandari ya Bagamoyo ni masharti magumu yaliyomo katika mkataba wa utekelezaji wa kazi hiyo.

Jiwe la msingi la ujenzi wa bandari hiyo liliwekwa na Rais mstaafu Jakaya Kikwete mwaka 2015 na ulitarajiwa kugharimu dola za Marekani bilioni 10.

Bandari hiyo endapo ingejengwa ingekuwa kubwa zaidi Afrika Mashariki ikiwa na ukubwa wa ekari 3,000 na viwanda 190 vingejengwa.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) uliowashirikisha wafanyabishara kutoka wilaya 139 nchini, Rais Magufuli aliweka wazi sababu za kusitishwa kwa ujenzi wa bandari hiyo.

Rais Magufuli alisema "kwenye mkataba wa ujenzi wa bandari hiyo kulikuwa na vipengele vya ovyo".

Rais Magufuli alisema mojawapo ya masharti ni kutojengwa wala kuendelezwa kwa bandari yoyote kuanzia eneo la Tanga hadi Mtwara.

"Yaani kwenye eneo lote kuanzia Tanga hadi Mtwara kusijengwe bandari yoyote. Bandari ya Kilwa tusiiendeleze, Bandari ya Mtwara ambayo itawezesha mikoa ya kusini kupokea mafuta badala yake Dar es Salaam kisha yarudi huko, hatutakiwi kuiendeleza, Barabara kutoka Mtwara hadi Bamba Bay ambayo itatuwezesha kusafirisha mizigo hadi Msumbiji tusiijenge," alisema Rais Magufuli.

Alisema sharti lingine ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutotakiwa kwenda kukusanya ushuru wala kodi katika eneo lile na walitaka wapewe hakikisho la miaka 33.

Pia alisema wawekezaji hao wangeweza kumiliki ardhi kwa hati ya miaka 99 pamoja na kutoruhusiwa kuuliza nani anamiliki eneo hilo.

Rais Magufuli alisema sharti lingine ni gharama zitakazotumiwa na mwekezaji huyo katika ujenzi wa bandari hiyo kutakiwa kurejeshwa.

# Samia ashangaa wadhibiti kuwa wakusanya mapato

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amezishangaa taasisi za udhibiti kugeuka vyanzo vya mapato.

Samia alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam mbele ya Rais John Magufuli wakati wa mkutano uliofanyika Ikulu baina yake na wafanyabiashara nchini.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Samia alisema taasisi hizo zimeacha kufanya kazi zao za udhibiti na badala yake zimekuwa vyanzo vya mapato kwa sababu sheria zilizoundwa zimeonyesha pale kuna makosa, wao wanadhibiti lakini ikitokea makosa inatakiwa kulipa tozo au faini.

"Badala ya kufanya udhibiti wao wameelekea zaidi kwenye vyanzo vya mapato. Kuna mmoja amesema hapa viwanda vinafungwa bila maelekezo, walioundwa kwa madhumuni ya udhibiti wafanye udhibiti, walioundwa kwa madhumuni ya tozo basi wafanye kazi yao," alisema.

Samia alisema yako mengi yanayofanyika na wafanyabiashara wanapohoji wanaambiwa ni maagizo kutoka juu.

"Sasa huko juu ni wapi? Ni vyema kila mtu akafanya kazi yake badala ya kuingilia kazi ya mwingine," alisema.

Kuhusu mazingira alisema anakubaliana na wafanyabiashara kuwa liko tatizo.

"Ni muhimu biashara zenu zikafuata mtiririko wa maelekezo ya mazingira, lakini taasisi ambazo zinatakiwa kufanya hivyo, ikiwamo NEMC

INAENDELEA UK. 8

# Akwepa jela kwa kulipa mil. 5/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imemhukumu kulipa faini ya Sh. milioni tano au kwenda jela mwaka mmoja John Chuwa (28), mkazi wa Tabata Barakuda baada ya kukiri kosa la kuchapisha maudhui katika mtandao wa Youtube bila kibali kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Maira Kasonde, baada ya mahakama yake kujiridhisha bila kuacha shaka kwamba mshtakiwa amekiri makosa yake hivyo inamtia hatiani.

Alisema kwa kuwa mshtakiwa amekiri makosa yake na kwamba hajaisumbua mahakama, anatiwa hatiani kwa kosa hilo.

"Mshtakiwa utalipa faini ya Sh. milioni tano na ukishindwa utakwenda jela kutumikia kifungo kwa mwaka mmoja," alisema Hakimu Kasonde.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alilipa faini hiyo na kuachiwa huru.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ajitetee ili apunguziwe adhabu.

Chuwa alidai kuwa mama yake mzazi, wadogo zake wawili wanamtegemea, hivyo akipewa adhabu ya kwenda jela watapata taabu.

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Elizabeth Mkunde, ulimsomea mshtakiwa maelezo ya awali kwamba 2018 mshtakiwa alifungua mtandao wa Youtube kwa kutumia barua pepe ya jalifilmstz@gmail.com.

Mkunde alidai kuwa mshtakiwa alitoa matangazo ya filamu za Kitanzania kupitia simu yake ya mkononi aina ya Huawei Y9 huku akijua hana kibali cha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alipokamatwa alikutwa na simu mbili za mkononi Huawei na Nokia. Mshtakiwa alikiri maelezo yote.

Mkunde alidai kuwa kwa sababu mshtakiwa amekiri makosa yake mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa katika terehe tofauti kati ya 2018 na Aprili 2019 jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alichapisha maudhui kupitia mtandao wa Youtube uitwao Charles Kombe bila kibali kutoka TCRA.

Mshitakiwa huyo aliposomewa shtaka lake alikiri kutenda kosa hilo na alichiwa kwa dhamana hadi jana alipohukumiwa adhabu hiyo.

# Mwalimu afa kwa kunywa gongo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MWALIMU wa Shule ya Sekondari ya Matemanga wilayani Tunduru, Hekima Gregory, maarufu kwa jina la Mvomela (49), amefariki dunia baada ya kunywa pombe ya kienyeji aina ya gongo. Wakati mwalimu huyo alipoteza maisha, watu watatu wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kukutwa na lita 3.5 za pombe hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa, alisema jana kuwa tukio la kwanza lilitokea Juni 5, mwaka huu, majira ya saa 3:00 asubuhi.

Alisema taarifa juu ya tukio hilo, ilitolewa kwenye kituo cha polisi cha Matemanga kutoka kwa Mratibu Elimu Kata ya Matemanga, Rashidi Nasoro.

Marwa alisema katika taarifa hiyo Nasoro alieleza kuwa mwalimu Gregory alikutwa akiwa anakunywa pombe aina ya gongo na inadaiwa kuwa alikuwa hajapata chakula.

Alieleza zaidi kuwa baada ya kumkuta mwalimu huyo akiwa chakari, hatua ya kwanza ilichukuliwa kwa kumpeleka katika hospitali ya misheni ya Kiuma ambako alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu.

Kwa mujibu wa Kamanda Marwa, mwili wa marehemu umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali hiyo ukisubiri kuchukuliwa na ndugu zake. Alisisitiza kuwa katika historia yake inadaiwa kuwa inaonyesha ilikuwa kawaida yake kunywa pombe hiyo kwa kuzidisha bila kupata chakula cha kutosha licha ya kuonywa mara kwa mara na viongozi wake.

Katika hatua nyingine, Kamanda Marwa alilitaja tukio lingine la kupatikana na pombe aina ya moshi ambalo alisema lilitokea Juni 4, mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana Mtaa swa Mlingoti Kata ya Majengo.

Alisema askari polisi wakiwa doria waliwakamata Suweni Athumani (44) mkazi wa Majengo, Juma Athumani (49) mkazi wa kijiji cha Kidugaro na John Raphael (44) mkazi wa Majengo, wote wakiwa na lita 3.5 za pombe aina ya gongo ambazo zilikuwa zimehifadhiwa kwenye chupa za plastiki za maji zikiwa zimefukiwa chini ya ardhi kisha kufunika nyasi nje ya nyumba.

Alisema watuhumiwa wote wamekamatwa na katika mahojiano ya awali, imebainika kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakijihusisha na uuzaji pamoja na unywaji wa pombe hiyo haramu.

Kamanda Marwa alisema watuhumiwa hao bado wako mahabusu na wanaendelea kuhojiwa kabla ya kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakifakamia mishkaki na ndizi choma, zilizokuwa zikiuzwa katikati ya barabara ya Mtaa wa Nyamwezi, Kariakoo, jana bila ya kuchukua tahadhari za kiafya kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu katika Jiji hilo. **PICHA: JOHN BADI**

# Mwanafunzi kidato nne alivyojinusuru kuozwa

**Na Consolata Evarist,** GEITA

LICHA ya Serikali kupiga vita mimba na ndoa za utotoni, hali imekuwa tofauti kwa mzazi Kwiyeyema Malongo, baada ya kutaka kumkatisha masomo na kumlazimisha kuolewa binti yake wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Lwamgasa wilaya na Mkoa Geita, kwa mahari ya ng'ombe sita na mbuzi wawili.

Tukio hilo lilibainika baada ya mwanafunzi huyo kutoa taarifa ya siri kwa walimu wake kwamba mzazi wake anataka kumuozesha, na amepokea mahari na kumwambia kwamba kwenye ukoo wao watoto wa kike huwa hawasomi bali huolewa na kuleta mali katika familia.

Binti huyo mwenye umri wa miaka 16, alitoa taarifa kwa waalimu ili wamsaidie kupinga kitendo cha baba yake, na aliwaambia walimu kuwa kama wangeshindwa kumsaidia angejiua ili kukwepa aibu ya kuolewa akiwa na umri mdogo kwa kuwa bado anapenda kusoma na kutimiza ndoto zake. Kwa mujibu wa mwanafunzi huyo, siku ya tukio la mahari wazazi walimzuia kwenda kufanya mtihani wa utimilifu (Mock), na kuwa walimsisitiza kufanya vibaya ili asiweze kufaulu. "Nilikua namalizia kufanya mtihani uliokuwa umebaki wa Kemia wakasema leo tunakupeleka kwenda kuolewa kwa hiyo nikifika shule niwadanganye waalimu naumwa, nasikia kizunguzungu nakuzimia ili walimu wanipe ruhusa nirudi nyumbani wanipeleke kuolewa," alisema.

Alisema walimu walifanya jitihada za kumsaidia baada ya wazazi wake kumfuata shuleni ili kumuombea ruhusa ya kumpeleke nyumbni akatibiwe, badala yake walimu waliita polisi na afisa elimu alikuja wakawakamata.

Alisema kwa sasa hana msaada wowote kutokana na familia yake kumtenga kwa madai ya kukataa kuolewa na kusababisha baba yake kukamatwa na Polisi.

"Hata ukoo wote umekasirika, wanasema mimi ndie niliesababisha baba akaenda jela kwa sababu nimekataa kuolewa... nataka nisome wamekaa wanasema kwamba mimi nimekataa kuolewa najifanya nasoma sana shule au mimi ndo msomi sana," alieleza.

Makamu mkuu wa shule hiyo, Masaguda Bundu, alisema mwanafunzi huyo ana nia ya dhati ya kusoma na wao baada ya kuletewa taarifa waliamua kumsaidia kwa siri sana bila wazazi kujua ndipo waliwawekea mtego wa kuwanasa siku walokua wamepanga kumpeleka mtoto wao kuolewa. "Taarifa tuliipata kwa usiri kwamba kuwa kuna watu nyumbani na baba yake anashuhudia katika kumlazimisha kuozeshwa katika namna ile."

"Sisi tuliendelea kufuatilia ukweli wa taarifa hizo na binti tulimpatia mawasiliano ili atupe taarifa za kila hatua watakayokuwa wamefikia, maana walikuwa wakimzuia mara kwa mara kuja shuleni,"alisema Bundu.

Afisa Elimu wa Sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Richard Mwakihaba, alisema watu wanne wanashikiliwa na Jeshi la Polisi akiwamo baba wa mwanafunzi pamoja na baba wa kijana ambaye alitaka kuozeshwa pamoja na shangazi na kaka wa muoaji.

# Washukuru JPM kuwakumbuka

**Na Mary Geofrey,** BUCHOSA

WANANCHI wa kijiji cha Nanyara, Halmashauri ya Buchosa, wilayani Sengerema mkoani Mwanza, wamempongeza Rais John Magufuli (pichani) kupitia Mamlaka ya Bandari (TPA), kwa kujenga gati katika Bandari ya Lushamba kwa ajili ya kurahisisha usafiri.

Tangu mwaka 1958, wakazi wa kijiji cha Buchosa na vitongoji vya Mwibale, Msikitini, Kisarazi na Gembale, walikuwa wanaunganishwa na usafiri wa mitumbi ambayo ilikuwa ikiishia majini lakini baada ya kujengwa gati hilo watapata unafuu na kuondokana na adha walizokuwa wa wanapata.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Lazaro Ngonzo, akizungumza na waandishi wa habari, waliofika katika bandari hiyo jana kwa ajili ya kuona maendeleo ya mradi huo, alisema kwa miaka 61 tangu kuanzishwa kwa bandari hiyo, hakukuwa na gati linalorahisisha usafiri wa kwenda visiwani.

"Tunamshukuru Rais John Magufuli kwa kuruhusu ujenzi wa bandari hii, hakika tumekumbukwa kwa sababu bandari hii itarahisisha usafiri wa kwenda visiwani kwa urahisi tofauti na sasa tunapata shida," alisema.

Alieleza adha wanazopata wakazi hao zaidi ya 8,000 wa kijiji hicho ni usafiri wa mashaka, kupanda boti ndani ya maji hali inayosababisha kupoteza mali zao na kulazimika kuvua nguo wakati wa kupanda na kushuka.

Alisema kwa siku jumla ya boti 13 zinatoa huduma za kwenda na kurudi katika visiwa vinavyozunguka kijiji hicho.

"Tunaishukuru Serikali, ujenzi wa bandari hii ni msaada mkubwa kwetu, tunaamini Serikali imetuona na imetufikia, matatizo yetu yanakwenda kumalizika sasa," alisema Ngozo.

Mtendaji wa kijiji hicho, Benjamin Ndungwizi, alisema licha ya kurahisisha usafiri pia bandari hiyo ambayo inategemewa na wakazi 8,798, itatoa ajira kwa vijana wa maeneo yanayozunguka kijiji.



Aidha, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kulinda miundombinu ya bandari hiyo kwa sababu wote ni wanufaika.

Naye mmoja wa wananchi katika Kijiji cha Kanyala, Charles Shuka, mbali na kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa bandari hiyo, aliiomba Serikali kupeleka kivuko cha kuwavusha.

Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Victoria, Geofrey Lwesya, alisema mradi wa ujenzi wa gati la bandari hiyo, umegharimu Sh. bilioni 1.265 ambazo ni fedha za ndani.

Alisema ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 90 ya kazi ya utekelezaji na kwamba sehemu iliyobaki ni kumalizia ujenzi wa jengo la abiria, jengo la mizigo, uzio, vyoo, mnara wa tanki la maji na chumba cha mashine ya umeme.

"Ujenzi wa bandari hii ndogo, nzuri na ya kisasa imejengwa kwa viwango vya kimataifa, tunategemea wananchi wengi zaidi kuitumia bandari hii kwa manufaa yao mara itakapokamilika mwezi Julai," alisema.

Kwa upande wake Mhandisi wa TPA Ziwa Victoria, Abraham Msina, alisema gati hilo lina urefu wa mita 6.

"Mradi huu ni wa mwaka mmoja na tunategemea mkandarasi kuukabidhi Julai 9, mwaka huu na hatutegemei kuongeza muda," alisema.

# Wananchi watakiwa kulinda miundombinu

**Na Said Hamdani,** LINDI

WANANCHI wanaopelekewa huduma ya Nishati ya Umeme Vijijini nchini kupitia mpango wa (REA), wamesisitizwa kujali na kuthamini miradi wanayopelekewa kwa kuacha tabia ya kuhujumu miundombinu.

Ushauri huo ulitolewa na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Nishati Vijijini (REA), Dk. Andrea Komba, alipokuwa akizungumza kwa nyakati tofauti na wakazi wa vijiji vya Litama na Chinongwe "A" na "B" Wilaya ya Ruangwa.

Alisema Serikali kwa inatumia fedha nyingi katika kupeleka miradi ya maendeleo kwa wananchi, lakini Jambo la kusikitisha kumekuwa na hujuma nyingi zinazofanywa kwa kuharibu miundombinu ya nishati ya umeme na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali.

Dk. Komba aliwaambia wananchi hao kwamba zipo hujuma za umeme wakati serikali inatumia fedha nyingi, huku akiutaja mradi huo unaotekelezwa na Kampuni ya State Gred Ltd katika Mkoa wa Lindi pekee, unatumia zaidi ya Sh. bilioni 30 hadi kukamilika katika awamu ya sasa, na kwamba kiasi hicho si kidogo kwa kuwa ni fedha nyingi.

Alisema Serikali imeweka fedha hizo kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi, waweze kupata umeme,ili waondokane na maisha ya ujima wa kutumia vibatari na nyasi.

"Maeneo mengi ambayo tunatekeleza miradi yetu tunakuta nguzo zinadondoshwa, huku nyaya zikiibwa, na wakati mwingine unakwenda hadi unalipua transfoma ambazo tunazinunua kwa gharama kubwa," alisema Dk. Komba.

Pia, alisema ili umeme huo uweze kuwafikia watu wengi kwa manufaa yao na vizazi vijavyo, ni vyema kwa wananchi hao wakailinda miundombinu hiyo, ikiwamo kuacha kuchoma moto ovyo na njia zinazotumika kupitia nyaya za umeme.

## KIBONDO DISTRICT COUNCIL

**Tender No. LGA/041/HQ/WSDP/2018-2019/W/ Lot 1-2**

For

1. CONSTRUCTION OF WATER SUPPLY AND CIVILS WORKS FOR KIBONDO URBAN WATER BY USING TWABAGONDOZI BOREHOLE.

AND

2. CONSTRUCTION OF WATER SUPPLY AND CIVIL WORKS FOR KIBONDO URBAN WATER BY USING KUMWAYI BOREHOLE.

**Invitation for Tenders**

**Date: 04th June ,2019**

1. The Government of United Republic of Tanzania has set aside funds for the operation of the Kibondo District Council during the financial year 2018/2019. It is intended that part of the proceeds of the fund will be used to cover eligible payment under the contract for water supply and civil works for Kibondo urban water by using Twabagondozi and Kumwayi Borehole in Kibondo District Council.

2. The Kibondo District Council now invites sealed tenders from eligible Contractors registered as civil contractors class VI and above for carrying out the works as provided in the BOQs found in Tender Documents, the works to be done are as follows:-

**WORKS TO BE DONE**

| TENDER NUMBER | TENDER NAME | CONTRACTOR'S TYPE |
|---|---|---|
| LGA/041/HQ/W SDP/2018-2019/W/01 | CONSTRUCTION OF WATER SUPPLY AND CIVILS WORKS FOR KIBONDO URBAN WATER BY USING TWABAGONDOZI BOREHOLE. | Civil contractor class VI and above |
| LGA/041/HQ/W SDP/2018-2019/W/02 | CONSTRUCTION OF WATER SUPPLY AND CIVIL WORKS FOR KIBONDO URBAN WATER BY USING KUMWAYI BOREHOLE. | Civil contractor class VI and above |

3. Tendering will be conducted through the National Competitive Tendering (NCT) procedures specified in the Public Procurement Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

4. Interested eligible Tenders may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of T***he Secretary of Kibondo District Council Tender Board on behalf of Kibondo District Council tender board P.O.Box 43, Kibondo from 08:00 am to 03;30pm*** on Mondays to Fridays and public holidays inclusive.

5. A complete set of Tendering Document(s) in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 4 above and upon payment of a **non-refundable fee of Tshs: 200,000.00.** Payment should be made to Revenue Accountant of Kibondo District Council ***after being given the control number.***

6. All tenders must be accompanied with photocopy of the following Documents:
   - Bid Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.
   - Current Business Licence of relevant works
   - TIN number of the company
   - Certificate of Registration with CRB.
   - Current receipts of CRB.
   - Bank Statements of current three Conservative months.
   - Special Power of Attorney whose holder must be an employee of Company or whose name appears in the Company profile.
   - VAT registration Certificate
   - Schedule of work.
   - Proposed plants owned or hired by the firm to execute the project.

7. All tenders in one original plus two copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below: The Secretary of Kibondo District Council Tender Board, P.O Box 43, Kibondo at or before 10:30am local time on Monday 18th of June, 2019. Tenders will be opened promptly thereafter at 12:00 Pm local time in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening ceremony at Kibondo PMU'S Offices.

8. Late Tenders, Portion of Tenders, Electronic Tenders, Tenders not received, Tenders not opened and not read out in public at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**RUTEMA D.M**
**District Executive Director**
**KIBONDO DISTRICT COUNCIL.**

215265002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Amunike, nyota Stars wanahitaji kuaminiwa*

**KIKOSI** cha wachezaji 32 wanaounda Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars), kiliondoka nchini kuelekea Misri kwa ajili ya kuendelea na mazoezi ya kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019).

Fainali hizo zinazoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) zinatarajiwa kuchezwa kuanzia Juni 21 hadi Julai 19 mwaka huu kwa kushirikisha timu 24.

Taifa Stars ni moja kati ya timu zilizofuzu kucheza fainali hizo, na imepangwa katika Kundi C ikiwa na nchi za Senegal, Algeria na majirani zetu kutoka Afrika Mashariki , Kenya maarufu Harambee Stars.

Katika kujiweka imara kabla ya kuanza kwa fainali hizo, Taifa Stars inatarajia kucheza mechi mbili za kirafiki za kimataifa dhidi ya wenyeji Misri na Zimbabwe.

Mechi hizo mbili za kirafiki, ni moja ya sababu ya kikosi cha Stars kuamua kwenda mapema Misri, ili kuanza kuzoea hali ya hewa ya nchi hiyo ambayo ni tofauti na iliyoko jijini Dar es Salaam, mahali ambapo 'askari' wa Tanzania walianza kujinoa.

Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko na mitazamo tofauti baada ya Kocha Mkuu wa Stars, Emmanuel Amunike, kutangaza wachezaji wanaokwenda Misri, ikiwa ni mchujo wa awali.

Wakiwa Misri, Mnigeria huyo atafanya tena mchujo na kubakisha idadi ya wachezaji 23 ambao ndio wanatakiwa kusajiliwa kwenye michuano hiyo, kama kanuni za CAF zinavyoelekeza.

Nipashe linawataka wadau kumpa ushirikiano Amunike ili aweze kuiongoza vema timu hiyo kama alivyokuwa akipambana katika safari ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo, ambazo Watanzania tulizikosa kwa miaka 39.

Kumekuwa na maoni tofauti baada ya kocha huyo kutangaza kuwaacha nyota sita, katika mchujo wa awali akiwamo, nahodha na mshambuliaji wa Yanga, Ibrahim Ajibu na kiungo wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Jonas Mkude.

Amunike ndiye kiongozi mkuu wa benchi la Stars, uwezo wake ndio ulifanya akapewa dhamana ya kuiongoza timu hiyo, hivyo anatakiwa kuungwa mkono kwa ajili ya kupambana na kupata matokeo chanya kwenye michuano hiyo ambayo atakutana na vigogo wa Afrika Magharibi.

Kama wadau wataendelea kuona uamuzi wa kuwaacha Mkude na Ajibu, haikuwa sahihi, hali hiyo inaweza kuwavunja moyo wachezaji ambao wamebakia kwenye kikosi hicho, wakashindwa kupambana kutokana na kuonekana hawana uwezo ukilinganisha na nyota hao waliotemwa.

Amunike ameweka wazi kuwa yeye ataendelea kuamini kwamba mchezaji bora ni yule mwenye uwezo wa juu na mwenye nidhamu, bila ya kuzingatia anatoka timu gani, na kufunguka zaidi kuwa sifa hizo ni baadhi ya vitu vilivyomfanya yeye apate nafasi ya kucheza soka katika klabu kubwa ya Barcelona huko Hispania.


Kama wadau wataendelea kuanza kuwagawa wachezaji, hilo linaweza kupunguza morali kwenye kikosi hicho ambacho kinasubiriwa kuwapa burudani Watanzania ambao kwa muda mrefu walikuwa watizamaji.

Gazeti hili linawaomba wadau wa michezo na hasa wa mpira wa miguu kumpa ushirikiano Amunike pamoja na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kufanikisha Stars kufanya vema katika fainali hizo na si kusindikiza timu nyingine.

Kila la kheri Taifa Stars, Kila la kheri Tanzania. Afcon 2019 Ni Zamu Yetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# *Usishue dau na maji yajaa*



Na Barnabas Maro

**IBRAHIM** Ajibu, usiteremshe au kuvuta dau majini ikiwa maji yamejaa. Methali hii ni muhimu kwako kukufunza umuhimu wa kutenda jambo wakati ufaao ili usije kujihatarisha au kujiletea maangamizo.

Ajibu, wahenga walisema "Bahati ikibisha hodi sharti ufungue mlango mwenyewe." Yaani jambo la kheri likikufika wapaswa kulifurahia. Hii ni methali ya kuwanasihi au kuwashauri watu (wewe ukiwa mmoja wao) wanaopata nafasi nzuri ya kujifaidi lakini wakacheleachelea au kutoitaka!

Husemwa "Mcha bahari hapendi safari" maana yake mtu anayeogopa bahari hapendi kusafiri.Twanasihiwa kwamba tudhamiriapo kulifanya jambo tusiwe na uchelewevu, ajizi ya kulikabili au tusiwe na woga.

Zipo habari kwamba Ajibu anawaniwa na Simba, timu aliyoiacha na kujiunga na Yanga msimu uliopita na sasa mkataba wake umefikia ukomo. Yasemekana kapewa kiasi fulani cha fedha na bilionea wa Simba, Mohammed Dewji "MO" ili kumrejesha 'kundini' katika klabu hiyo iliyotwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa pili mfululizo.

Wakati huo huo, timu maarufu ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), pia ilitangaza nia ya kumwania kijana huyo kutokana na uwezo wake wa kulichezea gozi la ng'ombe kama utakavyo na kuwaburudisha watazamaji wa timu yoyote unayoichezea. TP Mazembe ni moja ya timu maarufu zaidi Afrika inayomilikiwa na bilionea mwenye machimbo ya madini nchini humo.

TP Mazembe ndio iliyomfungulia mlango Mbwana Samatta anayechezea timu ya KRC Genk ya Ubelgiji na kusababisha wenyeji wamwite 'Samagoal' kwa jinsi anavyofunga mabao hata kuiwezesha timu yake kutwaa ubingwa wa ligi nchini humo.

Samatta ni zao la Simba kisha TP Mazembe na sasa KRC Genk ya Ubelgiji aliyoiwezesha kutwaa ubingwa huku akiibuka mchezaji bora wa mwaka mwenye asili ya Afrika kati ya wachezaji wote wanaocheza kandanda nchini Ubelgiji.

Thamani ya Samatta imevuka nje ya Ubelgiji kwa kutajwa kutakiwa na timu za Watford, Leicester City na Burnley za Englanda.

Kuna habari kuwa timu ya Aston Villa inamhitaji Mtanzania huyo kwa udi na uvumba na imemtengea pauni milioni 12 za Uingereza, sawa na Shilingi bilioni 40 za Tanzania! Mbali ya timu za Uingereza zinazomhitaji Samatta, pia kuna timu za FC Roma ya Italia na Lyon ya Ufaransa.

Simpingi Ajibu kujiunga na timu yoyote aipendayo kwani "kipenda roho hula nyama mbichi." Roho ikipenda huweza kula hata nyama mbichi. Pia kitu anachokipenda mtu au inachokipenda roho ya mtu huwa ni kama dawa yake. Methali hii hutumiwa kumpigia mfano mtu anayeelekea kukipenda kitu sana ingawa wengine wanakiona kuwa kibaya.

Masikini na umasikini wake hulala fofofo akimwachia Mungu matatizo yake yote. Siku zote Mungu yuko moyoni mwake akisema: "Kupata kuna Mungu ukikosa shukuru." Maana yake kukipata kitu au kukikosa ni mapenzi ya Mungu. Twapaswa kumshukuru japo hatukupata.

Ajibu anapaswa kutambua kuwa mchezaji anayecheza kandanda Ulaya ana faida mbili kubwa, kwanza anapata ujuzi na ufundi zaidi wa mchezo huo unaopendwa sana duniani. Pili, mshahara anaolipwa hauwezi kulinganishwa na mshahara anaolipwa mchezaji yeyote humu nchini hata wale wanaotoka nnje ya Tanzania.

Ni rahisi tu kuangalia maendeleo ya Samatta tangu ajiunge na klabu ya KRC Genk. Amejenga jumba lake la maana kule Kigamboni jijini Dar es Salaam, pia anajenga Msikiti utakaowasaidia waumini wa dini ya Kiislamu kufanya ibada zao.

Kama hiyo haitoshi, sasa Samatta anashirikiana na msanii Ali Kiba kukusanya fedha ili kuwasaidia watu wasiojiweza. Huu ni mwaka wa pili timu za wachezaji hao zikicheza jijini Dar es Salaam na mara zote timu ya Samatta imeondoka na ushindi mnono dhidi ya timu ya Ali Kiba. Mwaka ujao mchezo wao utahamishiwa mkoa utakaotajwa baadaye.

'Auni' ni kitendo cha kumsaidia mtu mwingine ili aondokane na matatizo; msaada, muawana. Sikuamini kama Watanzania ndivyo tulivyo linapokuja suala la kuwasaidia wenzetu wasiojimudu! Mchezo ule haukuwa wa kuwanufaisha Samatta na Kiba, bali kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye uhitaji.

"Katika mambo yote nimewaonesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, 'Ni heri kutoa kuliko kupokea!'" (Matendo 20:35).

Sichukii Ajibu kwenda Simba wala sifurahii kuendelea na Yanga, kinachonisikitisha ni yeye kutojitambua. Hakuna anayependa kuishi maisha yale yale mpaka mwisho wa dahari (milele) bali hutaka kuwa na maisha bora zaidi.

Ajibu, achana na ushabiki wa Simba na Yanga, kajiunge haraka na TP Mazembe ili ujifungulie njia ya kwenda ng'ambo utakakopata maendeleo na maisha mazuri zaidi kuliko kuzing'ang'ania Simba au Yanga. Kokote utakapokwenda ugenini, acha lelemama na uvivu.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**



Wajumbe wa kamati maalumu ya kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wa Malawi, anaotumia bandari ya Dar es Salaam wakikagua miundombinu katika bandari kavu ya Malawi iliyopo jijini Mbeya jana, ili kuhamasisha matumizi zaidi ya bandari hiyo kupunguza siku za kusafirisha mizigo kwenda Malawi. **PICHA: IDDY MWEMA**

# Watalii milioni 1.4 kuja nchini

**Novatus Makunga,** ARUSHA

IDADI ya watalii watakaoingia nchini kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 inatarajia kuongezeka kutoka milioni 1.3 hadi milioni 1.5.

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasa, aliyasema hayo jana mjini hapa alipokuwa akifungua Maonyesho ya Kimataifa ya Utalii yanayofahamika kama Karibu-Kili Fair.

Hata hivyo Kanyasu alitoa angalizo kwamba mafanikio ya sekta ya utalii, yanategemea zaidi ushiriki wa sekta binafsi ambayo alisema ndiyo mdau mkubwa wa serikali katika kuendesha utalii kwa mafanikio.

"Maonyesho haya ya Kili-Fair yana nafasi kubwa ya kutangaza masoko ya utalii nchini katika mataifa mbalimbali endapo yatatumiwa vizuri na kuongeza nchi zaidi ya za sasa zipatazo 45," alisema.

Alisema maonyesho haya ni muhimu katika kutangaza masoko ya utali wa Tanzania na kwamba mwaka jana washiriki 370 walihudhuria.

Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Nape Nnauye, alipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuwa na utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi katika kutangaza vivutio mbalimbali vya utalii.

Nnauye ambaye pia ni Mbunge wa Mtama alisema maonyesho haya ni muhimu katika kukuza utalii, hatua ambayo alisema itaongeza mapato ya serikali.

Alisema kama kuna sheria ambazo ni kikwazo katika sekta hiyo, ni vyema zikawasilishwa katika kamati yao ili kujadiliwa na Bunge kwa lengo la kuzifanyia marekebisho.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Devota Mdachi, alisema katika hatua ya kukuza na kuongeza idadi ya watalii, mwezi ujao Tanzania inatapokea kundi kubwa la watalii 200 kutoka katika Jimbo la Hong Kong nchini China.

"Kundi hili litakuwa kundi la pili baada ya kundi la kwanza la watalii, wafanyabiashara na wawekezaji 336 waolifika nchini Mei, mwaka huu," alisema.

Naibu Balozi wa Ujerumani nchini, Jorg Herrera, alisema nchi hiyo imekuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono jitihada za Serikali katika masuala ya uhifadhi wa wanyamapori Alisema katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, serikali ya Ujerumani imetoa zaidi ya Euro milioni 100 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya uhifadhi, maji na afya kwa serikali ya Tanzania

# Walalamikia gharama kubwa kufuata matibabu nje ya mkoa

**Na Restuta Damian,** KARAGWE

BAADHI ya Wananchi wa Kata Kihanga wilayani Karagwe mkoani Kagera, wameeleza changamoto ya upataji wa matibabu ya magonjwa sugu kutumia gharama kubwa kufuata matibabu katika hospitali za rufani.

Walisema gharama kubwa za kufuata matibabu hayo nje ya mkoa ni kikwazo kutokana na uchumi wa vijijini kuwa mdogo na hutegemea kipato kitokanacho na kilimo.

Omary Ajunila, mkazi wa kijiji cha Mramba, alisema kwa miaka mitatu amekuwa akikabiliwa na changamoto ya ugonjwa wa moyo kupanuka, hali inayomfanya kulazwa katika kituo cha afya kwa ajili ya kupatiwa dawa.

Alisema kama huduma za tiba zingekuwa karibu zingesaidia kupunguza gharama ili kujiokoa na kurejesha afya yake kuwa imara kuendelea na shughuli za uzalishaji wa kilimo mashambani.

"Ingewezekana serikali kutusogezea huduma za madaktari hata kwenye mkoa wetu

INAENDELEA UK. 8

# Chato wanza kunufaika na bandari

**Na Mary Geofrey,** CHATO

BANDARI ya Nyamirembe, wilayani Chato mkoani Geita, inatarajiwa kuanza kufanya kazi, mara baada ujenzi wa gati ya kisasa unaogharimu Sh. bilioni 4.1 kumalizika Agosti mwaka huu.

Kwa kipindi cha miaka nane, meli ziliacha kutia nanga katika bandari hiyo, kwa sababu kampuni iliyokuwa inatoa huduma kusitisha, hivyo kukamilika kwa ujenzi huo, kutaiwezesha Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), kuanza rasmi kutoa huduma.

Mhandisi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Ziwa Victoria, Abraham Msina, alisema mradi huo unaendelea na umefikia asilimia 40 utekelezaji.


Alisema bandari hiyo itakapoanza kazi itachochea biashara katika mikoa mbalimbali na nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda.

"Meli zilizokuwa zinatoka mikoa ya Mwanza, Kagera, Musoma na nchi jirani zilikuwa zinatia nanga, lakini kwa miaka nane kampuni iliyokuwa inatoa huduma iliacha kwa sababu meli zake ziliharibika. Hivyo baada ya TPA kukamilisha kazi ya ujenzi huu, MSCL wataanza rasmi kutoa huduma za meli," alisema Msina.

Alieleza kuwa, mradi wa ujenzi huo unafanywa na mkandarasi wa ndani ambaye ni Kampuni ya VJ Mistry, kutoka Bukoba mkoani Kagera.

Msina alisema sehemu ya kazi iliyobakia ni kumalizia ujenzi wa gati, jengo la abiria, jengo la mizigo, chumba cha mashine ya umeme, vyoo na chumba cha walinzi. Mwakilishi wa mkandarasi wa mradi huo, Injinia Anderson Mbogowe, alisema wanatarajia kukamilisha kazi hiyo Julai mwaka huu na kuukabidhi kwa Serikali Agosti mwaka huu.

"Kazi inaendelea vizuri na tunatarajia tutamaliza ndani ya muda tuliokubaliana na Serikali, hivyo Agosti tutakabidhi kazi hii," alisema.



# Ataka wawekezaji wafanye mambo ya tija

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Baraza la Biashara la China na Tanzania, Xian Ding, amewataka wawekezaji wanaokuja kuwekeza nchini kuhakikisha uwekezaji unaofanyika unalenga kuacha ujuzi kwa wazawa ili kusaidia nchi kukua kiuchumi na kimaendeleo.

Ding aliyasema hayo jana baada ya wanafunzi, wafugaji na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kutembelea kampuni ya Huatan Investment Group iliyoko Pugu Kinyamwezi, ambayo huzalisha vyakula vya mifugo kwa kutumia malighafi za nchini.

Kampuni hiyo imekuwa ikitoa elimu bure kwa wazawa na wanafunzi ambao wanataka kuingia kwenye ujasiriamali wa ufugaji kwa kuwafundisha namna ya ufugaji bora na vyakula vinavyopaswa kulishwa mifugo hiyo ili wahusika wapate faida.

Akizungumza baada ya kupokea ugeni huo, Ding alisema endapo wawekezaji wataacha ujuzi kwa wazawa, wataisaidia Tanzania kukua kiuchumi na maendeleo kwa haraka badala ya kuwekeza viwanda ambavyo wazawa hawatashiriki moja kwa moja kupata fursa.

"Azma ya kuifanya Tanzania kufikia uchumi wa viwanda kama ambavyo Rais John Magufuli anavyotekeleza sasa ni jambo nzuri sana ambalo litafanya nchi kukua kimaendeleo," alisema.

Alisema kampuni hiyo ni sehemu ya wanafunzi wa vyuoni na shule mbalimbali za msingi na sekondari kwenda kujifunza bure namna ya kuzalisha chakula cha mifugo ili iwasaidie pindi watakapomaliza masomo yao na kuingia kwenye ujasiriamali. "Wanafunzi wakipata mafunzo haya tunayotoa bure tunaamini watakaporudi kwenye jamii wataendeleza elimu hii na kufungua viwanda vyao wenyewe, tunawaomba wajitokeze kwa wingi kujifunza," alisema. Meneja wa kiwanda hicho, Matucha Magerengo, alisema mbali na kampuni hiyo kuzalisha vyakula vya mifugo, pia inajihusisha na ufugaji wa kuku kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo ni sehemu ya mafunzo kwa wanaofika hapo.

"Leo (jana) tumetembelewa na wana chuo, kikundi cha wafugaji wa ng'ombe na TIC ambao wamejionea uzalishaji wa chakula cha mifugo na ufugaji wa kuku kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo husaidia kutokuwa na vifo vitokanavyo na magonjwa," alisema.

# Samia ashangaa wadhibiti kuwa wakusanya mapato

INATOKA UK. 3

(Baraza la Mazingira la Taifa) haikuwa ikifanya vizuri. Tumeanza kuibadilisha NEMC, tumechukua hatua kadhaa. Tuliunda kamati kuangalia utendaji wa NEMC tukagundua makandokando yaliyomo," alisema na kuongeza:

"Ninavyowaambia kuna watu si chini ya watano wapo mikononi mwa Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), wanaotoka NEMC na idara yetu ya mazingira ndani ya ofisi yangu," alisema.

Samia (pichani) alisema wamepanga upya timu zao na kuelekeza kazi za kufanya, hivyo NEMC itabadilika hatua kwa hatua na kufika kunakotakiwa na kuwataa wafanyabiashara nao watunze mazingira.

Kuhusu tozo za mazingira alisema watu wa NEMC walikuwa wanafanya vibaya kuchukua fedha kutoka kwa wafanyabiashara na kuahidi kulisimamia vizuri.

Akizungumzia katazo la mifuko ya plastiki ambalo utekelezaji wake umeanza mwanzoni mwa mwezi uliopita na serikali kuruhusu aina nyingine ya plastiki ziendelee kutumika, Samia aliwataka wafanyabiashara kupitia sheria, kanuni zilizotolewa ili yale yaliyoruhusiwa waendelee nayo na kuchukua tahadhari ya mifuko ilisoruhusiwa.

**MAJALIWA AKOLEZA**

Awali, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alisoma karatasi aliyotoka kwa mmoja wa wafanyabiashara ambayo ilieleza kuwa wafanyabiashara walioalikwa Ikulu jana wanaogopa kuisema TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) kwa sababu wakitoka hapo watashughulikiwa walikotoka.

"TRA ni miungu watu wanakuadhibu kwa kodi kubwa alafu wanataka na rushwa na ukishindwa duka linafungwa, ukihoji wanasema ni maagizo kutoka juu. Sijui ni wewe, au makamu au Rais?" Majaliwa alisoma ujumbe huo kutoka kwenye katarasi iliyomfikia.

Majaliwa alimweleza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, na Kamishna Mkuu wa TRA, Charles Kichere, kuwa baada ya mkutano huo, asikute mtu aliyeadhibiwa kutokana na maelezo aliyotoa jana.

"Hawa wameitwa maalum kuja



kuishauri serikali. Yeyote aliyetamka mambo yake changamoto za serikali, TRA ni chombo cha serikali, watu wote waliosema wasiadhibiwe," alisisitiza.

# Watumishi wa TRA kushtakiwa kwa rushwa

INATOKA UK. 3

Rais Magufuli alipohoji idadi ya wahusika na kujibiwa kuwa walikuwa ni watatu ndipo alipoamua kutoa maagizo hayo dhidi ya watumishi hao watatu.

"Wote watatu washikwe wawekwe ndani halafu wapelekwe mahakamani, wakiwa mahakamani Kamishna wa TRA wasimamishe kazi, lazima ifike mahali watu tujifunze vizuri, TRA mkapige hesabu kwa sababu biashara ya huyu mfanyabiashara imekaa ndani kwa muda wa miaka mitatu mumlipe fidia," aliagiza Rais Magufuli.

Awali, akizungumzia kuhusu tukio hilo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema mfanyabiashara huyo alikamatwa mwaka 2016/2017 na mzigo wake ulirudishwa juzi kwa sababu aliyemkamata aliomba rushwa na yeye alikataa kutoa.

"Huyu mfanyabiashara alikataa kutoa rushwa na alikubali bora mzigo ukae huko huko, siku alipokuja kueleza nashukuru kamishna wa kodi ya ndani ambaye ni mgeni TRA nilipomuagiza amshughulikie, alitekeleza na siku ya pili alisema ni kweli mfanyabiashara ameonewa , tukaagiza arudishiwe mzigo, tabia hii kamishna wa TRA ipo huko ndani," alisema.

Aliongeza: "Walipomkamata alikataa kutoa rushwa usiku aliokamatwa, walipomkamata alisema fedha ninayo ipo nyumbani, wakamsindikiza hadi Kariakoo nyumbani kwake, walipofika yule mfanyabiashara aliwaambia rushwa hatoi wakitaka wamuue.

"Kwa bahati nzuri kulikuwa na polisi waliokuwa kwenye doria, wakaangalia kuna nini wakaona kuna mgogoro nadhani wana bohari, walipompeleka, mzigo wake umekaa miaka mitatu amerudishiwa mwaka huu mwezi wa nne."

# Walalamikia gharama kubwa kufuata matibabu

INATOK UK. 7

wakatupatia matibabu ya kuponya magonjwa nadhani ni wengi wenye kuhitaji hata gharama ikawa kidogo kulipia tukiwa ndani ya mkoa badala ya kwenda Muhimbili au Bugando," alisema Ajunila

Kaumbya Nzilamula, mkazi wa Kijiji cha Kapanda, alisema amekuwa akisumbuliwa na miguu kujaa maji, tatizo lilitokea baada ya kujifungua kizazi cha tatu na hadi sasa ni miaka sita anatibu maumivu. Nzilamula alisema anashindwa kupata huduma ya matibabu kutokana na hali yake ya kiafya kutomwezesha kwenda nje ya mikoa pamoja na gharama kubwa.

Kwa upande wake Mratibu wa Chama cha Urafiki kati ya Tanzania na China, alisema kutokana na changamoto ya jiografia, wananchi wa Karagwe wamekuwa wakisumbuka kuwaona wataalamu wa afya wanaokwenda katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera kutoa huduma.

Kahama alisema kupitia changamoto hiyo, chama hicho kimeanza kutoa matibabu kwa wananchi hao lengo ni kuisaidiana Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jinsia, Wazee na Watoto kutoa huduma ya afya kwa jamii yenye uhitaji mkubwa wa madaktari bingwa. "Niseme tu hata kama mtu awe na bima kuifuata huduma katika meneo ya Bugando, Muhimbili, Moshi bado ni changamoto kubwa kwani lazima atatumia pesa ya kujikimu huko ...sasa hiyo inawakwamisha watu wengi kufuata huma hivyo, naishukuru sasa tumeipata faida kwa huduma ya afya kutufuata tulipo," alisema Kahama.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Dk. Marco Mbata, alisema magonjwa yanayoripotiwa kwa wingi kwenye hospitali hiyo ni moyo, mifupa, magonjwa ya wanawake, tezi dume, macho, kinywa, meno, magonjwa ya watoto.

## Mawaziri watatu wachongewa

INATOKA UK. 3

Neema Nyerere, mkulima, alisema kuna urasimu mkubwa wa kupata mikopo ya kilimo.

Naye, Sauli Amon, Mbunge wa Rungwe Magharibi, alisema kuna utitiri wa kodi kwenye bidhaa za vipodozi, mamlaka zaidi ya sita zinakata kodi kwenye bidhaa moja.

Agustino Makoye, mfanyabiashara wa mafuta kutoka Mwanza, alisema kuna tozo zaidi ya 20 kwenye mafuta, na kamba ushuru wa bidhaa umekuwa ukikusanywa na maofisa walioshika bunduki.

Sylvanus Buyaga, mmiliki wa kiwanda cha Bora Mkoa wa Dar es Salaam, alisema sekta ya ngozi imekuwa na matatizo makubwa, ngozi imekuwa ikikusanywa nyingi, lakini hakuna sehemu ya kuipeleka.

"Tunazalisha viatu vya majeshi mwaka wa tatu sasa, lakini jeshi halikununua kwetu bali linaendelea kuagiza viatu kutoka nje, kwenye stoo yetu tuna jozi ya viatu zaidi ya 5,000, tumeandika barua wizarani, lakini hatupewi majibu," alisema Buyaga.

Dk. Abbas Tweve kutoka sekta ya misitu, alisema sekta ya misitu ina utitiri wa kodi zipatazo 19 zinazotozwa na halmashauri.

Zubeir Madie kutoka Kigoma, alisema soko la dagaa na samaki , pamoja na vituo vya mafuta mkoani Kigoma vinakufa kwa sababu ya utitiri wa kodi. Alisema urasimu wa TRA ndiyo ulioua biashara mkoani Kigoma. Hussein Nasoro kutoka Geita, alisema wafanyabiashara wanakwepa kulipa kodi kwa sababu ya usiri uliopo TRA.

Alisema mzigo mmoja wenye thamani sawa unaoagizwa na wafanyabiashara watatu tofauti unatoza kodi tofauti unapofika bandari ya Dar es Salaam.

Tox Kihansi kutoka kiwanda cha mbolea cha Minjingu, alisema wanazalisha tani 150,000, lakini serikali bado inaagiza mbolea kutoka nje.

Mbunge wa Geita, Joseph Kasheku Musukuma, alisema wafanyabiashara wengi hawamjui Waziri wa Viwanda na Biashara, hawatembelei wafanyabiashara na kujua matatizo yao.

Paschal Kihanga kutoka Morogoro, alisema viwanda vingi vimekufa Morogoro kama cha kutengeneza magunia kwa sababu ya uagizwaji wa mifuko kutoka nje ya nchi.

Alisema hata kiwanda cha Tumbaku nacho kipo hatarini kufungwa, na ifikapo mwakani kitakuwa kimeshafilisika kwa sababu ya utitiri wa kodi.

# Ujerumani wafundisha Watanzania mafunzo kwa vitendo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Fachakademien cha nchini Ujerumani, wameshiriki mafunzo kwa vitendo kwa kuwafundisha wanafunzi wa Shule ya Tarangire Pre & Primary English Medium ya Mjini Babati, mkoani

Manyara, kufanikisha ushirikiano na uhusiano mwema.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Tarangire, Eva Mrutu, akizungumza jana alisema wamefarijika kupata ugeni huo, kutoka nchini Ujerumani ambao kwa namna moja au nyingine umewaongezea ujuzi wanafunzi wao.

Mrutu alisema wageni hao wamewafundisha wanafunzi wao mambo mapya ambayo walikuwa hawajafundishwa.

"Wanafunzi wetu wamefurahi kupata mambo mapya, ikiwamo michezo na nyimbo mbalimbali ambazo hawakuwahi kuziimba, zimewaongezea morali ya kusoma zaidi," alisema Mrutu.

Mmoja kati ya wanafunzi hao wa Chuo Kikuu cha Fachakademien, Rebecca Steve, alisema hii ni mara yake ya kwanza kufika Tanzania na amefurahishwa na

ukarimu ulioonyeshwa kwao.

"Tutarudi tena hapa nchini Tanzania kwani watu wake ni wakarimu, wema na wenye upendo kwa wageni, kwa hakika tunefurahi mno kufika hapa Shule ya Tarangire," alisema Rebecca.

Mwanafunzi wa darasa la nne kwenye shule hiyo ya Tarangire, Jackline Peter alisema walimu hao kutoka nchini Ujerumani, walimfundisha kuchora na kuchanganya rangi.

Mwanafunzi wa darasa la tatu, Philipo Tabari, alisema alifurahia nyimbo mpya walizofundishwa ikiwamo wimbo wa tembo ni mnyama mzuri.

Mwalimu wa kitengo cha masoko, Judith Misana, alisema shule yao ipo kwenye miteremko ya Mlima Kwaraa mjini Babati, barabara kuu ya Mamire, karibu na Chuo cha Veta Manyara.

"Wazazi na walezi tunawakaribisha wote waleteni watoto wapate elimu nzuri hapa kwetu Tarangire, kupitia kaulimbiu ya shule yetu ya juhudi katika kutafuta elimu na Mungu," alisema Misana.

Alisema shule hiyo ina walimu wazuri wenye kufundisha masomo bora, mabasi ya kusafirisha wanafunzi kila siku, vyakula vizuri wanavyolima wenyewe na sehemu nzuri za kulala.



Sehemu ya wanafunzi wa shule ya awali na msingi ya New Light ya Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoa wa Manyara, wakiwa shuleni jana, wakati wa kufungwa kwa nusu muhula wa mwezi wa Juni. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kampuni yatoa ufafanuzi wa malalamiko ya wananchi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KAMPUNI ya utengenezaji wa vinywaji vikali aina ya K Vant ya Mega Beverage Co.LTD mkoani Arusha, imetoa ufafanuzi wa malalamiko ya wananchi kuhusu kiwanda hicho kilichopo kwa Morombo, kutiririsha maji machafu kwenye makazi ya watu wakati mvua.

Akizungumza na waandishi wa habari kiwandani hapo, Msimamizi wa kuhakiki ubora wa bidhaa kutoka kampuni hiyo, Gisella Shirima, alisema kuwa maji

yanayotoka kiwandani hapo kwenda mto wa jirani, hayana madhara kwa kuwa mamlaka husika zimeyapima maji hayo na kujiridhisha kuwa hayana madhara kwa binadamu.

Awali wakazi wa eneo la kwa Murombo, walidai kuwa kiwanda hicho kimekuwa kikitiririsha majitaka, yanayofunguliwa nyakati za alfajiri mvua zinaponyesha na wanayaelekeza kwenye makazi ya watu jambo ambalo walidai yanahatarisha afya zao.

Shirima aliwatoa hofu wananchi pamoja na wakazi hao wanaopakana na kiwandani hicho, wanacho kibali kutoka Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC ), kinachowaruhusu kuelekeza majitaka kwenye makazi ya watu, baada ya kujiridhisha kuwa hayana madhara.

Aliongeza kuwa pia wana kibali kutoka kwa Msimamizi wa mabonde ya maji Pangani, kinachothibitisha kuwa maji hayo, yanayotoka kiwandani hapo

kwenda mto jirani hayana madhara yoyote kwa viumbe hai na pia yanaweza kutumika kwa shughuli zingine za kibinadamu kwa kuwa hayana kemikali.

"Haya maji yanayotoka kiwandani hayana madhara yoyote kwa sababu yanatumika kuoshea chupa na hayana kemikali yoyote inayochanganywa , hivyo hayawezi kuleta athari kwa binadamu," alisema Shirima.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, James Kimaro, alisema kuwa kiwanda hicho hakina tatizo na majirani zake kwa kuwa wamekuwa wakishiriki hata katika shughuli za maendeleo kwa wananchi ikiwamo kutoa huduma bure ya majisafi yanayopatikana kiwandani hapo.

Alisema mbali na huduma hiyo, wananchi pia wametoa ajira kwa wananchi wanaoishi pembezoni na kiwanda hicho jambo lililozidisha ujirani mwema.

# Wakumbushwa kuchagua viongozi watakao watumikia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANANCHI wameaswa kuchagua viongozi wenye hofu ya Mungu katika chaguzi za serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao wenye nia njema ya kuwatumikia bila ubaguzi wa rangi, kabila au dini.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Monaban Trading and Farming ya jijini hapa, Dk. Philemon Mollel, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza katika Baraza la Eid el Fitr, lililofanyika jana katika Taasisi ya Zawiyatul Qadiriyyat iliyopo Ngarenaro jijini hapa.

"Ndugu zangu mkumbuke karibuni tutakuwa na uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani, tukumbuke kuchagua viongozi

watakaotutumikia na kujali shida zetu sio unachagua mtu anayekwenda kujinufaisha mwenyewe huyo hatufai," alisema.

Pia alisema inapendeza ndugu wakae pamoja kwa amani na upendo na kukumbuka kuwasaidia watu wenye mahitaji maluum katika jamii wakiwamo masikini, yatima, wajane na wazee wasiojiweza, kwa kuwa hawakupenda kuwa katika hali hiyo.

Alikemea baadhi ya tabia ambayo wamekuwa nayo baadhi ya watu kwa kuwa na dharau na kuwanyanyapaa watu wenye mahitaji maalumu na kuwataka kutowatenga na kushirikiana nao, kwa hali na mali na kuacha kuwatenga kwa kuwa wao ni binadamu kama walivyo wengine.

Katika Baraza la Eid, Mollel alichangia lori kumi za mawe na Sh. milioni moja, kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kingo ya Mto Ngarenaro, ambao umekuwa ukileta adha kubwa kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Awali, Mwenyekiti wa Taasisi ya Twarika, mkoani hapa, Abdi Omar Bin Said, alisema Taasisi yake imejikita zaidi katika utunzaji wa mazingira kuhakikisha kuwa wanadhibiti kingo za Mto Ngarenaro kwa kupanda miti ambayo tayari wameshaanza.

Alisema pia Taasisi hiyo imejikita katika kutoa elimu katika fani mbalimbali, kwa lengo la kuwafanya vijana kupata elimu na ujuzi wa kujiajiri, ikiwa ni pamoja na kulea watoto yatima na wanaoishi

katika mazingira hatarishi, ambapo mpaka sasa wana vituo vitano.

Kwa upande wake mlezi wa taasisi hiyo nchini, Salum Darwesh, alisisitiza umuhimu wa umoja na upendo, miongoni mwa madhehebu yote ya dini.

"Ukiwa na afya njema utaweza kusimama na kutembea popote, ukiwa na kitu ni rahisi kusema chochote na kutoa msaada kwa wahitaji na endapo una utu utawajali wenzako kuwathamini na kuwapenda," alisema Darwesh.

# Aahidi wawekezaji Umeme siku 36

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, amewaalika na kuwaahidi umeme wa uhakika kwa mwaka mzima wa siku 365 kwa wawekezaji watakaojenga viwanda na kuwekeza mkoani humo.

Alitoa ahadi hiyo jana alipotembelea vituo vya kupoozea umeme mkoani humo, alisema lengo la ziara hiyo ni kupima na kutathmini endapo kutakuwapo na mazingira rafiki ya uwekezaji ndani ya mkoa huo. Alisema kuwa, umeme unaozalishwa katika mkoa wa Kilimanjaro unatosheleza na kuwataka wawekezaji wa viwanda kuja kuwekeza kwani hakutakuwa na tatizo la kukatika katika kwa umeme.

Mkuu huyo wa mkoa alilaani taarifa iliyotolewa na Meneja wa Tanesco Mkoa wa Kilimanjaro, mhandisi Mahawa Mkaka, ya kuwapo kwa baadhi ya watu kulihujumu shirika hilo kwa kuharibu kwa makusudi miundombinu na wezi wa nyaya za umeme na kuiomba jamii kutoa ushirikiano katika kuwaibua watu hao ili waweze kuchukuliwa hatua stahiki.

"Nasikitika kuona baadhi ya watu wanalihujumu shirika letu kwa kuiba umeme, wezi wa mafuta ya transfoma pamoja na nyaya za umeme. Nitoe wito kuwa mtu anayefanya matendo haya ya kuhujumu uchumi, atakapokamatwa ni lazima ashitakiwe kwa kuhujumu uchumi na wananchi tunaomba ushirikiano katika kuwabaini watu hawa," alisema Mghwira.

Akizungumzia suala la madeni wanayodaiwa na shirika hilo zikiwamo taasisi za umma na watu binafsi, Mghwira alisema kuwa, kauli ya Rais John Magufuli ya kukata umeme kwa wasiolipa ni muhimu na kuwataka kutekeleza agizo hilo.

Alisema taasisi za umma zimekuwa zikiua taasisi nyingine kutokana na kushindwa kulipa madeni yao na hilo alisema linafanyika kwa makusudi kwa sababu kama Tanesco ingekuwa shirika binafsi wangelipa madai na madeni hayo.

Aliwaambia wanaodaiwa kuanza kulipa kidogo kidogo na kuzitaja taasisi zinazoongoza kuwa na madeni makubwa kuwa ni Magereza na Polisi, alisema Mghwira.

Kwa upande wake, Meneja wa Tanesco mkoa wa Kilimanjaro, Mkaka alisema kuwa, umeme unaozalishwa ni megawati 135, na matumizi kwa mkoa mzima kwa sasa ni megawati 42.

Mkaka alisema kuwa, kwa miundombinu iliyowekezwa na shirika hilo katika mkoa huo ina nafasi ya kupata umeme wa kutosha hata kama wawekezaji wa viwanda watajitokeza hawatapata changamoto ya kukatika kwa umeme.

Alisema changamoto kubwa sasa ni madeni makubwa kutoka kwa wateja yakiwamo taasisi za umma. Meneja huyo alisema kuwa changamoto nyingine ni ulinzi wa miundombinu ya shirika hilo ambapo baadhi ya watu wasio waaminifu wamekuwa wakiharibu miundombinu, wakiiba nyaya za umeme mafuta ya transfoma huku wengine wakiiba vyuma na wizi wa umeme.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Josephat Torner Aid Europe Tanzania, Josephat Torner, akionesha kaulimbiu ya Siku ya Kimataifa ya Uelewa kuhusu Ualbino, inayotarajiwa kufanyika Juni 13 mwaka huu, wakati alipokutana na waandishi wa habari jijini Mwanza jana. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Wawakilishi 'mbumbumbu' watimuliwa mkutanoni

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWENYEKITI wa Bodi ya Shule ya Msingi Pasua iliyoko Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Shaban Machivya, amelazimika kuwatimua vijana waliotumwa kuwawakilisha wazazi kwenye kikao cha shule kwa maelezo kuwa hawawezi kuchangia mjadala wala hawana majibu ya changamoto zinazojitokeza. Alilazimika kuwatoa wawakilishi vijana kwenye kikao cha wazazi kwa kile kilichodaiwa kuwa ni wanashindwa kuchangia mjadala na kutoa changamoto zinazowakabili wanafunzi wa shule hiyo.

Uamuzi huo uliutoa jana kwenye kikao cha wazazi na walezi cha kujadili maendeleo ya wanafunzi na nidhamu zao shuleni watakapofungua mwezi ujao.

Alisema amelazimika kuwatoa wawakilishi hao vijana kwenye kikao cha wazazi kwani wamekuwa wakishindwa kuchangia hoja yoyote kwenye vikao wala kufanya maamuzi ya hatima ya wanafunzi hao. "Wazazi wamekuwa na kasumba ya kuwatuma wawakilishi ambao wakifika hapa wanashindwa kutoa maamuzi ya wanafunzi wanaosoma hapo. Wakati mwingine wazazi wanapokuja kushirikisha hukataa maazimio yaliyopitishwa na kikao hicho,"alisema na kuongezea:

"Tunapiga marufuku tabia hii ya kutuma wawakilishi kufika kwa ajili ya maendeleo ya watoto huku nyinyi mkienda kwenye shughuli zenu tunawaomba wazazi kuangalia misingi ya hawa watoto na kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa walimu ili tuweze kufikia lengo la kujenga kizazi imara," Kwa upande wake Ofisa Elimu , kata ya Bomambuzi, Emelinda Kyara, alikiri kuwapo kwa changamoto kwenye vikao kutokana na ushiriki mdogo wa wazazi kwa mambo muhimu ya yanayowahusu wanafunzi yakiwamo chakula nidhamu na maendeleo kwa ujumla. Alisema ikiwa mzazi hana dharura ni vyema akafika kwenye vikao ili kueleza changamoto zinazomkabili ili kuwapo urahisi wa kufanya maamuzi katika suala la makuzi na malezi ya watoto.

"Watoto hawa wanahitaji ushirikiano wa kutosha kati ya wazazi , walezi na walimu ili kuwajengea misingi imara. Tulijadili suala la chakula shuleni lakini wapo wazazi hawajalipa hadi leo na wanapokumbushwa hudai ya kuwa hawana taarifa.Hii ni mbaya na sisi kama viongozi hatutakubali jambo hili liendelee tena,"alisema

## Vijana watakiwa kujikomboa wasifikirie kupewa ajira

**Na Mary Mosha,** MOSHI

VIJANA wanaomaliza elimu ya juu wamekumbushwa tena kuacha kubweteka kusubiri ajira rasmi kutoka serikalini au sekta binafsi badala yake wabuni mikakati ya kujikwamua na umaskini na ukosefu wa kazi.

Mkurugenzi wa shirika lisilo kuwa la kiraia la Hand in Hand Eastern Africa, Steven Wambua, alieleza kuwa vijana wanaomaliza elimu ya juu ni wabwetekaji sugu wasiojishughulisha kujikwamua, wakifikiri kuwa ajira ndilo suluhisho la umaskini.

Wambua alisema hayo jana mjini Moshi wakati akizungumza na viongozi wa serikali pamoja na vikundi mbalimbali vinavyojishughulisha na shughuli za maendeleo katika jamii zinazowazunguka.

Alisema vijana ndiyo wanaongoza kwa umasikini kutokana na kukosa shughuli za kufanya hali inayopelekea wengine kujiunga na makundi ya kuhalifu ikiwamo dawa za kulevya wizi.

"Vijana wamekuwa wakibweteka kusubiri kuajiriwa baada ya kumaliza elimu ndiyo maana unaweza kukutana na msomi hana kazi ya kufanya anatangatanga mtaani," alisema Wambua.

Aliwaambia kuwa ili kuleta suluhisho la changamoto hiyo kwa vijana ,shirika hilo linalenga kukuza uchumi kwa kuwapa ujuzi na maarifa vijana na wanawake wanaoishi katika mazingira magumu ili waweze kuanzisha biashara zao wenyewe badala ya kusubiri kuajiriwa.

Kwa upande wake meneja wa mradi huo mkoani Kilimanjaro, Mshindi Isaya, alisema kwasasa shirika hilo lina miradi mikubwa miwili ukiwamo wa Hilt unaolenga kuwahudumia wakulima na wafugaji, na mradi wa Boeing ambao utawahudumia vijana.

Isaya, alisema takribani watu 2,000 wamewafikiwa katika vikundi 82 vilivyopo wilaya za Hai na Moshi.

Awali Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Moshi,Rose Minja, alisema vijana wanakabiliwa na changamoto ya mawazo potofu inayowapelekea kushindwa kujiunga na vikundi vya maendeleo.

"Vijana hawana mwamko wa kujiunga na vikundi wakidhani kuwa wanaotakiwa kufanya hivyo ni wakinamama hali inayosababisha kutangatanga bila shughuli za msingi,"alisema Minja.

Katika mkutano huo Justine Joseph, kutoka shirika lisilo la kiserikali la Restless, aliahidi kuwa shirika hilo linatarajia kutoa taarifa za tafiti za ushirikishwaji wa vijana katika shughuli za maendeleo.








Wananchi wakichagua mifuko mbadala ya plastiki kwa ajili ya matumizi mbalimbali katika eneo la Uhindini, jijini Dodoma jana. Serikali ilipiga marufuku mifuko ya pastiki tangu Juni Mosi mwaka huu, hivyo mifuko mbadala imekuwa ikinunuliwa kwa kasi kubwa licha ya kuwa na gharama kubwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana waonywa kukaa vijiweni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

RAIS wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Kanda ya Kati, Twaha Nyange, amewataka vijana wa kiislamu kufanya kazi kwa bidii badala ya kukaa vijiweni.

Nyange alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa sala ya Eid El Fitri iliyofanyika katika msikiti wa Makole Sabasaba, jijini hapa.

Alisema Taifa lolote haliwezi kuimarika bila kuwa na vijana wenye nguvu ya kufanya kazi, hivyo hakuna sababu ya kukaa bila kujishughulisha wakati wana uwezo wa kujiajiri wenyewe.

Aliwataka vijana kutekeleza kwa vitendo maagizo yote yaliyokuwa yakitolewa na viongozi wao ndani ya misikiti katika kipindi cha Mfungo wa Ramadhani ya kuhimizwa kufanya kazi kwa bidii na kutokuwa wasindikizaji kwenye maisha. “Kumekuwapo na tabia kwa baadhi ya vijana baada ya Mfungo wa Ramadhani wanarudia maovu yao bila kutambua kuwa wakifanya hivyo wanaharibu funga yao,” alisema.

Kwa upande wake, Shekhe Khaweja Muzaffar wa Jumuiya hiyo, aliwataka waumini kuishi maisha waliyoyaishi kipindi cha Ramadhani.

“Inasikitisha kuona baadhi ya waumini ambao walikuwa kwa kipindi chote cha mfungo huu wanageuka kwa kufanya vitendo viovu ambavyo havina faida zaidi ya hasara kwa familia husika na hata kwa serikali pia,” alisema.

# Wakurugenzi waagizwa kuboresha miundombinu

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

WAKURUGENZI wa halmashuari nchini wametakiwa kuhakikisha fedha wanazozikusanya kutoka katika vyanzo vyao mbalimbali zinatumika kuboresha miradi na miundombinu ya jamii ili kuchochea kasi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, wakati akiwa katika Shule ya Sekondari ya Wella iliyopo eneo la Mkonze.

Alisema wakurugenzi hao hawanabudi kutumia vizuri mapato inayoyakusanya kuboresha miradi ya maendeleo kwa kuwa serikali imedhamiria kutatua changamoto na kero mbalimbali kwa jamii. “Napenda kuwaagiza wakurugenzi wa halmashauri wahakikishe kuwa wanaelekeza fedha wanazokusanya katika kutatua changamoto zinazozikabili halmashauri zao badala ya kusubiri kero hizo zishughulikiwe na serikali kuu,” alisema.

Hata hivyo, Naibu Waziri huyo alisema bado kuna changamoto za ukosefu wa matundu ya kutosha ya vyoo, uchakavu wa miundombinu ya shule, na kero nyingine za aina hiyo zinaweza kutatuliwa kwa kupitia makusanyo ya halmashauri husika.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo alitembelea eneo la Dodoma Makulu ambapo alijionea namna kikundi cha vijana cha Jikomboe kinavyojishughulisha na ufyatuaji wa matofali, kikiwa ni miongoni mwa vikundi vilivyopata fedha za mkopo kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Pia Waitara alitembelea mradi wa kimkakati wa ujenzi wa soko na kituo cha mabasi wenye thamani ya Sh. bilioni 34.

Mkurugenzi wa Jiji hilo, Godwin Kunambi, alisema wana mikakati ya kutatua changamoto zinazozikabili shule za msingi na sekondari ambapo katika bajeti ijayo walitenga kiasi cha Sh. bilioni 8 ili kujenga miundombinu.

Alisema kuanzia sasa Jiji la Dodoma litahakikisha kuwa ujenzi wa shule zake utakuwa wa kisasa unaoendana na taswira ya makao makuu ya nchi.

Akizungumzia kuhusu changamoto zinazoikabili Shule ya Sekondari ya Wella ambayo majengo yake mengi hayajakamilika licha ya kuanza kutumiwa na walimu na wanafunzi wa shule hiyo, Mkurugenzi huyo alisema kwa mwaka huu jiji lilipeleka Sh.milioni 50 kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya miundombinu ya shule, na kwamba wanatarajia katika mwaka ujao wa fedha majengo yote ya shule hiyo yatakarabatiwa.

# Maambukizi VVU makubwa vijijini

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA.

IMEELEZWA kuwa hali ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa wananchi wa vijijini ni kubwa kuliko walioko mijini.

Hayo yalielezwa na Mratibu wa Mkoa wa Shirika lisilo la kiserikali la Tanzania Health Promotion Serpoty (THPS), Melikiory Massae, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Massae alisema uelewa wa wananchi wanaoshi maeneo ya vijijini kuhusu maambukizi ya VVU ni mdogo hali iliyosababisha kuongezeka tofauti na watu wanaoishi maeneo ya mijini.

“Shirika letu limekuwa likitoa elimu kuhusu kijikinga na maambukizi ya ugonjwa huo maeneo mbalimbali mjini na vijijini, lakini maeneo ya vijijini wamekuwa na uelewa wa chini sana tofauti na Mijini,“ alisema.

Alisema Shirika hilo linatoa elimu ya kujikinga na Ukimwi kwa kushirikiana na Serikali katika kata zote za Wilaya ya Kongwa na Dodoma Mjini.

Alibainisha kuwa baada ya kuzunguka katika kutoa elimu hiyo walibaini kuwa wananchi wengi wa maeneo ya vijijini wamekuwa hawachukui tahadhali katika kujikinga na maambukizi hayo.

“Kuna baadhi ya watu tulizungumza nao kuhusu hali ya kujikinga na Ukimwi wanaonyesha kutojali na wanashiriki ngono na watu wengi bila kinga yeyote,” alisema.


Aidha, alisema Shirika hilo limekuwa likitoa huduma ya kupima virusi vya Ukimwi na wakiwabaini walioambukizwa huwapeleka kituo cha afya kwa ajili ya kuanza kutumia dawa za kufumbaza makali ya ugonjwa huo.

“Kwa maeneo ya vijijini wamekuwa wakiweka kambi kwa muda na kutoa huduma ya kupima afya bure pamoja na ushauri nasaha kwa walioathirika,” alisema.

Massae alisema shirika hilo pia limekuwa likitoa elimu hiyo kwa makundi mbalimbali kama madereva wa malori, makahaba na watumiaji wa madawa ya kulevya.

Alitaja maeneo mengine wanayotoa elimu kuwa ni kundi la Wavuvi na watengeneza barabara kutokana na wengi kuwaacha wenza wao na kuhamia maeneo ya mbali.

Alisema Shirika linafanyakazi katika mikoa ya Dodoma, Simiyu, Arusha, Morogoro,Pwani, Mara, Mtwara, Shinyanga, Mwanza na Kilimanjaro.





# Mfumuko wa bei Zanzibar wapanda

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KASI ya mfumuko wa bei Zanzibar kwa Mei, mwaka huu, imeongezeka kufikia asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 2.9 kwa Aprili.

Pamoja na mfumuko huo kuongezeka, bei za vyakula na vinywaji visivyokuwa na vilevi zilishuka hadi asilimia 2.3 kutoka asilimia 3.3.

Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Bei katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Khamis Abdulrahman Msham, alisema faharisi za bei ziliongezeka hadi 110.9 kwa mwezi Mei ikilinganishwa na 107.6 kwa mwezi kama huo mwaka jana.

Alisema, kiwango cha mfumko wa bei za vyakula kilishuka hadi asilimia 2.3 kwa mwaka uliomalizikia Mei ikilinganishwa na asilimia 3.3 ya Aprili, mwaka huu.

Msham alisema faharisi za bei za vyakula ziliongezeka hadi 109.4 Mei, mwaka huu ikilinganishwa na 106.9 kwa mwezi kama huo mwaka jana wakati faharisi za bei kwa bidhaa zisizokuwa za vyakula ziliongezeka hadi 112.1 Mei mwaka huu kulinganisha na mwaka jana kipindi kama hicho.

Kwa upande wa bidhaa zisizokuwa za vyakula, mfumko uliongezeka hadi asilimia 3.6 Mei, mwaka huu ikilinganishwa na asilimia 2.6 ya Aprili, mwaka huu.

Alizitaja bidhaa zilizochangia kupanda kiwango cha mwaka cha mfumuko wa bei asilimia kwenye mabano kuwa zilikuwa mchele wa mapembe (13.9), unga wa sembe (1.4), unga wa ngano (2.6), ndizi za mtwike (37.3), ndizi za mkono mmoja (tano), sukari nyeupe (4.7), saruji (18, petroli (0.2) na dizeli asilimia 1.8.

Kwa upande wa mfumuko wa mwezi, alisema uliongezeka hadi asilimia 1.7 Mei, mwaka huu kulinganisha na asilimia 0.8 kwa Aprili, mwaka huu.

Naye Mhadhiri wa Uchumi kutoka Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Suleiman Simai Msaraka, alisema hali ya uchumi inaendelea vizuri na kinachohitajika ni uzalishaji wa bidhaa zaidi.

Meneja Msaidizi wa Uchumi kutoka Benki Kuu Tawi la Zanzibar, Moto Ng'winganele Lugobi, alisema pamoja na kasi ya mfumuko huo kuongezeka, bado Zanzibar imefikia hatua nzuri kulinganisha na malengo yaliyoweka ya kuwapo kwa tarakimu moja ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki.



Mjasiriamali akisukuma toroli lililobeba bidhaa zake, akielekea kwenye eneo lake la biashara katika eneo la Tazara, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wapewa somo kuwahudumia wazee

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa sekta mbalimbali za kijamii wameshauriwa kujenga ushirikiano wa karibu na wazee ili kuhakikisha jamii hiyo inapata huduma zote muhimu na kuimarisha ustawi wao.

Akizungumza katika mkutano wa wadau kuhusiana na ustawi na haki za wazee, Khalfan Salum Suleiman alisema wazee wa Zanzibar wanakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwamo usafiri, lishe duni, matibabu na makazi.

Alisema ili kuondokana na changamoto hizo, kuna umuhimu wa kujenga ushirikiano wa kisekta na kupanua wigo katika kuratibu, kufanya ushawishi pamoja na utetezi juu ya haki zao.

Aidha, alisema kuna umuhimu wa kujenga mtandao na kuunganisha nguvu katika mabaraza ya wazee kupitia shehia, ili kufanikisha azma ya kupigania haki za wazee. "Ili kufikia malengo tunapaswa kuhakikisha wazee wote waliofikia umri wa miaka sabini na kuendelea wanapata matibabu bora, usafiri nafuu, lishe bora na makazi bora," alisema.

Aidha, aliyataka mabaraza ya wazee katika shehia kuiga mfano wa baraza la wazee shehia ya Sharifumsa, lililowapatia wazeee wa sehia hiyo dirisha maalum la matibabu katika hospitali ye jeshi Mwanyanya.

Alisema kitendo cha wazee kupata dirisha maalum kunarahisisha upatikanaji wa matibabu, pia baraza hilo limefanikiwa kuishawishi wizara kuongeza dawa kwa ajili yao.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo walisema upatikanaji wa vitambulisho ndio njia pekee na suluhisho kwa wazee kupata huduma mbalimbali kwa wakati muafaka na kwa nafuu.

Walisema katika mazingira ya sasa imekuwa vigumu kwa wazee hao kupata huduma za afya kwa wakati, kwani wanapofika hospitali au vituo vya afya huwa hakuna dirisha maalum lililotengwa kwa ajili yao, sambamba na watendaji kushindwa kuwapa kipaumbele.

Aidha, walisema upatikanaji wa huduma za usafiri imekuwa changamoto kubwa kwao, kutokana na ukosefu wa vitambulisho maalum, hivyo kulazimika kupanda gari kwa kiwango cha bei anayotozwa abiria wa kawaida. Juma Resi kutoka shehia ya Kilimahewa alisema kumekuwa na wimbi la wazee kufariki dunia kutokana na ukosefu wa lishe bora, kunakochangiwa na sababu tofauti, ikiwemo ulaji wa kiwango kikubwa cha sukari pamoja na matumizi ya mafuta mazito. Aliishauri jamii, ikiwamo wazee kurudisha matumizi ya vyakula na mapishi ya asili pamoja na kudumu katika ulaji wa matunda na mboga mboga.

Mkutano huo uliozishirikisha sekta za ustawi wa jamii, afya, usafiri pamoja na masheha kutoka shehia mbali mbali za mkoa wa mjini magharibi, uliofanyika ukumbi wa CCM Wilaya ya Amani, uliandaliwa na Jumuiya ya Wazee Zanzibar (Juwaza) kwa lengo la kubadilishana uzoefu juu ya haki za wazee na kuondokana na changamoto zinazowakabili katika maisha yao ya kila siku.

# SMZ yapiga marufuku vyakula vya majimaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kudhibiti maradhi ya kuambukiza hasa kipindupindu, Wizara ya Afya Zanzibar, imepiga marufuku uuzwaji wa vyakula vya majimaji ikiwamo urojo na juisi za kutengeneza nyumbani.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya wa Wizara hiyo, Dk.Jamala Adam Taib, alisema wizara kwa kushirikiana Wizara ya nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, imejiandaa kufanya kampeni katika wilaya zote kufanya ukaguzi katika maeneo yanayofanywa biashara ili kudhibiti maradhi ya kuharisha.

Alisema hivi sasa wagonjwa tisa wa kuharisha wamepokewa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ambao wanatoka katika mitaa ya Chumbuni na Fuoni.

Dk. Jamala, aliwasisitiza wafanyabiashara kutofanya masihara katika jambo hilo kwa kuwa serikali itahakikisha mtu yoyote atakayebainika anavunja sheria na maagizo yaliyotolewa, anachukuliwa hatua.

"Sheria ya Afya na Mazingira inatupa nguvu hizo kwa hiyo hili halitakuwa na muhali. Tunaomba wafanyabiashara wafuate sheria vyenginevyo tusije tukalaumiana na kuonana wabaya," alisema.


Alisema wananchi wanapaswa kufahamu kuwa wako katika msimu wa mvua za masika na wizara inaendelea kutoa tahadhari na kufatilia kwa karibu kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa kipindi hicho ndicho huanza mlipuko ya maradhi ya kuharisha.

Pia alisema wizara ilianza kutoa tahadhari tangu mwezi wa Ramadhani watu wanavyotakiwa kufuturisha, vyakula vinavyotakiwa lakini baadhi walikaidi na kukiuka taratibu hizo na kufuturisha katika kumbi.

"Zaidi ya watu 100 walifuturishwa ambao hawajaja kwetu kupata miongozo na sisi kwenda kukagua. Watu walianza kuharisha kutokana na ukaidi wao," alisema.

Mtaalamu huyo aliwashauri wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ikiwamo kuchemsha maji kutumia vidonge vya 'water guard' na kunawa mikono kwa maji ya kutiririka kwa sabuni wanapotoka chooni na wakati wa kula.

Sambamba na hayo, aliwasisitiza wafanyabiashara wadogo kuzingatia suala la usafi wanapotengeneza vyakula vyao na kutumia juisi zinazotengenezwa viwandani.



Soma UK. 14
**BEN POL**

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI JUNI 8, 2019



# HAKUNAGA TENA
## RIHANNA ATISHA KWA NOTI

UK.19

BASI SAWA



## Msanii amlilia Ali Kiba

MSANII wa Bongofleva, Spince Seseme, amesema msanii mwenzake ambaye wamewahi kufanyakazi huko nyuma Ali Kiba hamkumbuki na mara nyingi amekuwa akimtupa kila anapomhitaji.
Akiongea kwenye kipindi cha Friday Night Live ya East Africa Television, Seseme ameweka wazi kuwa ameshamfuata mara nyingi Alikiba ili amsaidie hata kufanya kazi kwenye Label yake ya Kings Music lakini amekuwa hamsikilizi.
"Nishaenda sana kwa Alikiba lakini hanikumbuki ila kuna kupindi aliniomba msamaha mara tatu ila hata anapofanya show zake za mwisho wa mwaka hata hanialiki nimeamua tu abaki mshikaji kama kazi imeshindika", alifunguka Seseme.
Seseme alishirikiana na Alikiba kwenye ngoma inayoitwa Ayaya ambayo ilifanya vizuri sana mwaka 2012. Ngoma hiyo ilimtambulisha vizuri Seseme na mashabiki wakaamini atafanya poa lakini baadaye akapotea.



## Jay Moe hana mpango na youtube

MKONGWE wa muziki wa Bongofleva, Jay Moe, ameeleza kuwa huwa hasumbuliwi na mambo ya 'views' za ngoma zake kwenye mtandao wa Youtube ila anachozingatia yeye ni ujumbe utagusa wangapi.
Akizunguza kwenye kipindi cha Dadaz cha East Africa Television, Jay Moe amefunguka kuwa, wasanii kwasasa wanasumbuliwa na idadi ya watazamaji wa Youtube na sio ujumbe utawagusa watu wa jamii ambao hata hawajui mambo ya mtandaoni.
"Siangalii wimbo unapata views ngapi kikubwa ni 'content' gani inakwenda kwa jamii, unakuta ngoma yangu haijapata watazamaji wengi kwenye Youtube, lakini unakwenda sehemu za ndani ndani unakutana na mtu anakwambia anakufuatilia na ana wimbo wako", amefunguka.
Upande mwingine Jay Moe amesema kumekuwa na mambo mengi kwenye muziki na wasanii unakuta wanachukiana kisa hajapostiwa kwenye mtandao jambo ambalo sio la msingi sana.



# Ben Pol: Mchumba wangu anatumiwa sana sms

MKALI wa muziki wa kizazi kipya, Ben Pol, ameweka wazi kuwa kuna wasanii huwa wanamtumia meseji mchumba wake Anerlisa na mara nyingi huwa anaziona.
Akizungumzia hilo, Ben Pol amesema kuwa ameshawahi kukuta meseji za watu mbali mbali wakiwamo wasanii Shetta, Harmonize, na msanii wa Kenya Kaligraph Jones, lakini amekuwa hazitilii maanani.
"Nawaona, Shetta, Kaligraph, naona 'blue ticks' lakini sishangai kwa sababu ni msichana mrembo, na ukikaa naye kama hivi ndio unaona urembo wake", amesema Ben Pol.
Ben Pol kwa sasa yuko kwenye mahusiano rasmi na Anerlisa baada ya kumvisha pete ya uchumba, jambo ambalo mwenyewe anasema ni kitu kikubwa kwenye maisha yake.

## INSTA-TWITTER





**Kashindwa** jini kichwani utaweza we kibwengo mkaa baharini-**Riyama Ally.**



**Hakuna** kisicho na umuhimu na hakuna asiye na umuhimu. Asiekufaa kwa kanga atakufaa kwa chumvi. Hata mjinga ana umuhimu wake-**Snura Mushi.**



## Beka Flevour aachia video ya Dede

BAADA ya kimya kirefu, msanii Beka Flavour ameachia video ya ngoma yake aliyoipa jina la Dede.
Katika wimbo huo amemshirikisha mwanadada, Anitha ambaye ameonekana kuutendea haki vizuri zaidi.
Beka video yake hiyo mpya ameiachia Juni 5 mwaka huu na tayari imeonekana kupokelewa vizuri na mashabiki wake.
"Hii ni kazi yangu mpya, nawaomba mashabiki wangu waipokee vizuri kwani sijawaangusha," aliandika Beka kwenye ukurasa wake wa Instagram.




@burudanitele

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

UNASEMAAA...

# Johari amkwepa Ray

MCHEZA filamu wa Bongo Muvi, Johari, amesema hawezi kufanya kazi na Ray Kigosi kama ilivyokuwa zamani na mashabiki wake waache kufikiria mambo yaliyopita.
Johari amesema amerudi upya katika gemu na kwamba kazi zote anazofanya ambazo zinatarajia kutoka hivi karibuni zitakuwa na mambo mengi mapya.
"Mashabiki wasiwe na mazoea kwa kuona nafanya kazi na Ray, nimerudi nikiwa mtamu wasubiri kuona tamthilia na filamu zangu nyingine," amesema.



BODA 2 BODA

## Ommy Dimpoz
### anapoacha maswali mengi

WIKI hii mwanamuziki wa Bongo Fleva, Ommy Dimpoz, amevunja ukimya baada ya kutupia picha mtandaoni akionekana akiwa na kichanga.Picha hiyo ambayo aliiweka katika ukurasa wake wa instagram , imeibua mjadala mzito kutokana na msanii huyo kuweka ujumbe wenye utata, huku idadi kubwa wakisema kichanga hicho kinawezekana ni wake.
Ommy Dimpoz ambaye hapendi uweka mambo yake hadharani, aliandika ujumbe "Vipi Dengue Imeisha Nirudi nae? Haya Nafikiri yale Maswali ya unafanya nini Ulaya kila siku YAMEISHA"





## NEEMA YA MUNGU

Passcal Cassian anena mazito MSHINDI wa BSS mwaka 2009, Pascal Cassian , amewashukuru Watanzania kutokana na msaada wao waliompa katika kupigania maisha yake ambayo yalikuwa hatarini.Cassian akizungumza mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, amesema moyo wao wa kujitoa ndio ulimfanya kwenda nchini India na kupata matibabu ambayo yamemfanya kurejea afya yake kama ilivyokuwa awali.
"Nawashukuru Watanzania waliopaza sauti hadi Mkuu wa Mkoa akasikia na kunisaidia kiasi hiki ambacho kwangu nakiri kwamba sasa nimepona," amesema Cassian.Amesema kazi aliyoifanya kiongozi huyo ni kubwa na kwamba alipokwenda India mpaka aliporudi hakupata shida yoyote kiasi kwamba alijiona ni kama mtu wa kipekee."Naweza kutembea bila matatizo, sina shida yoyote kabisa ile mipira ambayo nilirudi nayo kutoka India imetolewa na daktari wangu kwa msaada wa wataalam wa India. Nathibitisha nimepona na naendelea kushuhudia maajabu makubwa ya Mungu," ameongeza

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Nishaweka** Sana lindo. hadi ulimbo. Wala hanati huyo mrembo-**Rich Mavoko**.



**Ubaya** ya njia za watu, viulize viatu-**Dogo Janja**.



**Tuwe** wakweli jamani. Hivi nani anaweza kuvumilia mapenzi ya mbali kati ya mwanamke na mwanaume?-**Queen Darleen.**

# Kuumbe!

**Na Adam Fungamwango**

YALISEMWA mengi, yakaandikwa mengi juu yake. Wengine wakaenda mbali zaidi na kusema 'jamaa huyu huenda si mzima.'

Huyu si mwingine bali ni msanii maarufu nchini, Ommy Dimpoz. Nadhani kwa sasa kitendawili kimeshaanza kuteguka. Juni 6 ameposti picha akiwa na kichanga kwenye kiwanja cha ndege cha Barcelona nchini Hispania.

Alikuwa amekilaza kwenye kigari na kukiburuza kwa mapenzi yote ya baba na mtoto.

Dimpoz alichapisha picha na kutuma video kwenye mtandao wake ya instagram akiwa na kichanga hicho, huku akikwepa kuandika chochote juu ya mtoto huyo, ingawa aliandika maneno machache kwa mtindo wa mafumbo.

"Vipi Dengue, imeisha nirudi naye? Hata nafikiri yale maswali ya 'unafanya nini Ulaya kila siku' yameisha."

Kwa maneno haya machache, baadhi ya watu wameshasema kuwa anayeonekana naye ni mtoto wake na ndiyo maana ameuliza kama ugonjwa wa dengue ambao unatingisha kwa sasa hata kwenye jijini la Dar es Salaam umeisha na amlete.

Lakini pia watafsiri wa maneno hayo yanasema kuwa yale maneno aliyoandika kuwa huwa anaulizwa anafanya nini Ulaya, majibu yake ndiyo yale ya kuonyesha mtoto, ina maana Ulaya ana demu na tayari amezaa naye.

Kama ni hivyo basi kwanza inabidi Dimpoz apate hongera yake.

Kwa kawaida msanii huyo amekuwa hana tabia ya kuweka maisha yake hadharani. Amekuwa akiishi maisha si ya siri, lakini hapendi mambo yake mengi kuwa hadharani na amekuwa na tahadhari kuwa kwa kila anachokifanya.


Baadhi ya wasanii wamekuwa na tabia ya kila wanachofanya kiwe kizuri au kibaya atafanya juhudi zote ili kitoke kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa ajili ya kujiongezea umaarufu.

Kwa jinsi ilivyo ni kwamba kumbe Dimpoz siku zote hizi alikuwa na demu wake Ulaya na amekuwa naye bila Wabongo kujua hadi amezaa naye na alivyowadizi watu kete ni yeye mwenyewe ameamua kuuweka mambo hadharani wala si 'mbea' yoyote yule kugundua hilo.

Huu ni mfano mzuri wa kuigwa na wasanii wote nchini, wakati mwingine si kila kitu cha kuweka hadharani.

Cha ajabu ni kwamba baadhi ya wasanii nchini yale mambo ambayo mashabiki wao wanahitaji wajue wao ndiyo wanaficha, lakini yale ambayo si muhimu yajulikane ndiyo wanataka kutumia nguvu kubwa kila mtu ayajue.

Dimpoz alitulia na kujua kuna wakati utafika ataamua kuweka mambo hadharani, na huu ndiyo wakati muafaka.



# DIMPOZ
## WA ULAYA, TOFAUTI NA BONGO

# WANAWAKE WA 5 WALIOTESA ZILIPENDWA

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni vigumu sana miaka ya nyuma kuona mtoto wa kike akijihusisha kwenye mausuala ya muziki.

Ilichukuliwa kuwa muziki uhuni, na kazi hiyo ya wahuni, au watu ambao maisha yao wanayajua wenyewe, hawana mbele wala nyuma na pia watu wasiojiheshimu.

Wazazi wengi hawakutaka watoto wao kujihusisha na masuala ya muziki, na hao ni watoto wa kiume tu, sasa fikiria kwa watoto wa kike inakuje?

Kwa maana hiyo hakukuwa na wanamuziki wengi wa kike kama ilivyo hivi sasa ambako kumekuwa na wimbi kubwa la wasanii wa kike.

Kwenye miaka ya 80, hadi mwishoni mwaka miaka ya 90, kulitokea wanamuziki waimbaji wachache wa kike ambao mbali na kuwa hawakuwa wengi, lakini waliwawakilisha vema wanawake wenzao kwa kufanya kazi hiyo kwa ustadi mkubwa, uwezo wa hali ya juu kiasi cha kujipatia umaarufu mkubwa nchini Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Na hao ndiyo walioanza kuondoa dhana ya kwamba mtoto wa kike akijiingiza kwenye muziki anakuwa amepotea.

Ndiyo walioanza kufanya wenzao nao kuona kuwa inawezekana, na mwanamke anaweza kufanya kazi ya muziki kama kazi nyingine yoyote, akajiheshimu na kuwa na familia yake, akaitunza na maisha yakaendelea. Hapo ndipo kikaja kizazi cha kina Luiza Nyoni (Mbutu), Jesica Charles, Hadija Mnoga 'Kimobitel', marehemu Amina Ngaluma na wengineo.

**Tabia Mwanjelwa**

Tunaweza kusema kuwa Tabia Mwanjelwa ndiye mama wa waimbaji wote wa kike nchini Tanzania.

Ndiye aliyefungua njia, kwani alianza kuimba kwenye miaka ya '80 akiwa na bendi mbalimbali kama Maquiz Du Zaire na King Kiki Double O.

Anakumbukwa sana kwa nyimbo zake kama 'Maisha ni Safari Ndefu', 'Jeni' alizozirekodi akiwa na Maquiz zinazopendwa hadi leo. Na wakati huo staili za uimbaji kwa wanawake ilikuwa ni kuiga ule wa Miriam Makeba, hivyo nyimbo hizo zina athari hizo.

Aliondoka mwishoni mwa miaka ya '80 na kwenda kuishi nchini Ujerumani, kabla ya kurejea nchini miaka ya hivi karibuni na amekuwa akifanya maonyesho kwenye bendi kadhaa, ingawa makazi yake ya kudumu ni huko Ulaya.

**Rahma Shally**

Ni mmoja wa waimbaji mwenye kipaji cha hali ya juu aliyepata kutokea nchini. Rahma Shally ni mwimbaji pekee wa kike ambaye amefanya kazi na bendi nyingi zaidi kuliko mwingine yoyote nchini. Naye pia aliathiriwa na uimbaji wa Miriam Makeba.

Hii ni kutokana na bendi nyingi kumkubali na kutaka kufanya naye kazi. Amepigia bendi za Mwenge Jazz Band, Vijana Jazz, Sambulumaa na nyingine nyingi.

Aliimba nyimbo kama 'Naomba Tuheshimiane' akiwa na Mwenge Jazz, 'Kaka Saddy' akiwa na Vijana Jazz, pia 'Zamaradi' akiwa na Sambulumaa na nyingine nyingi. Alifariki dunia mwanzoni mwa miaka ya '90.

**Emma Mkello**

Alikuwa ni mwimbaji wa kike ambaye hakuathiriwa na uimbaji wa Miriam Makeba. Emma alikuwa na uimbaji wake tofauti kabisa akiwa na sauti nyembamba na nyororo mno, kuliko Rahma Shally au Tabia Mwanjelwa. Huyu alikuwa ni mke wa mwanamuziki maarufu kabisa wakati huo Eddy Sheggy. Hata sauti walifanana yeye na mumewe. Nyimbo kama 'Milima ya Kwetu', 'Kichekesho', 'Hesabu Miaka' na nyingine nyingi akiwa na Super Rainbow, pia "Umbea Sipendelei' aliouimba kwa ustadi wa hali ya juu akiwa na Tanzania Stars 'Watunjatanjata' utunzi wake Ally Choki ulimfanya kuwa bora na maarufu zaidi. Alifariki dunia katikati ya miaka ya '90.

**Nana Njige**

Huyu alikuwa ni mwimbaji wa kike ambaye alikuwa na sifa nyingine zaidi ambayo ni urembo.

Alijaaliwa urembo uliowashangaza na kuwapumbaza wanaume wengi wakati huo. Hata jina lake la Nana Njige likageuza likawa 'Nana Mzuri.' alipigia bendi mbalimbali kama Super Rainbow na Tancut Almasi na mwishoni kabisa alipigia bendi ya Magereza. Huko anakumbukwa sana alipoimba wimbo uliovuma sana uitwao 'Ashura.' Naye alifariki dunia katikati ya miaka ya '90.

**Kida Waziri**

Mwishoni mwa miaka ya '80 kuliibuka kipaji cha ajabu kutoka kwa mwanadada Kida Waziri. Aliitingisha nchi kwa vibao kama 'Wifi Zangu Mna Mambo', 'Penzi Haligawanyiki' sehemu ya kwanza na ya pili, 'Wivu' na nyingine nyingi akiwa na bendi ya Vijana Jazz Band.

Nyota yake ilififia ghafla baada ya kifo cha kiongozi wa bendi hiyo, Hemed Maneti ambaye pia ni mzazi mwenzake mwaka 1990. Kwa sasa anaendelea na shughuli zake nyingine kwa ajili ya kuendesha maisha yake.



Kida Waziri

# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.

**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0682 808 694**



# Ndoano Siri inayoficha mengi

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA ina mambo mengi. Hakuna siri ya watu wawili , Siri pekee inaweza kustirika ni ya mtu mmoja pekee pale akiamua asimwambie mtu yoyote yule.

Kwenye maisha ya ndoa inatakiwa kuwapo na amani, faraja na uvumilivu. Yeyote yule kati ya mke na mume akitaka kuingiza vitu vingine ambavyo vipo nje ya uwezo wao wa kawaida, badala yake viko kwenye uwezo wa Kimungu, ndoa hiyo itakuwa kwenye misukosuko na kufa kabisa. Hata kama itaponyeka ni kwa kudura tu za Mwenyezi Mungu. Kutopata mtoto hakuwezi kusababisha ndoa kuyumba kwa sababu wanandoa hawapangi mtoto, badala yake ni majaaliwa tu ya Mungu.

Haya ndiyo yaliyojitokeza kwenye filamu hii ya 'Ndoano'. Stanley Msungu ndiye kinara wa filamu hii.

Msungu na mkewe wanaishi kwa amani na utulivu kwenda ndoa yao iliyojaaliwa kupata mtoto mmoja wa kike aitwaye 'Suzan'. Lakini kuna siku moja binti yao alitoweka nyumbani, Msungu akamtafuta na kumkuta na jamaa mmoja wakiwa dukani akinunuliwa vitu. Akajitambulisha kama baba wa mtoto huyo, jamaa akaondoka. Anapomwambia wajihi wa mtu aliyemkuta na mtoto wao, mkewe anashtuka.

Wiki moja baadaye mtoto anatekwa na watekaji wanampigia simu baba yake wakihitaji jumla ya Sh Milioni 10. Kazi ya kuzitafuta pesa hizo inachukua muda, lakini zinapatikana na mtoto anarudi nyumbani.

Miezi kadhaa tena mtoto anatekwa na zinatakiwa Sh Milioni 5. Nani anayefanya kazi hii? Kwa nini? Na chanzo ni nini?

Baada ya kukaa miaka kadhaa bila kupata mtoto, mke wa Msungu alikuwa na wasiwasi na ndoa yake. Shoga yake akamwambia aende hospitali kupima ili kuonekana kama ana matatizo. Hakuonekana nayo, hivyo moja kwa moja mwenye mapungufu atakuwa ni mumewe.

Kwa ushauri wa shoga yake ni kwamba asimwambie mumewe, bali anamtafute mwanaume ampe mimba na mtoto ambambikie mumewe. Anatafutwa mwanaume mmoja anaiwa Julio. Anaifanya kazi yake ipasavyo kwa mkataba wa kulipwa pesa. Hivyo ndivyo mtoto Suzan alivyopatikana.

Ni Msungu tu ambaye hajui kinachoendelea. Julio analipwa Sh Milioni 5, lakini tano zingine zinachelewa na jamaa alipotishia kutoa siri, mama anafanya kila njia analipa.

Tamaa ya pesa inawaingia Julio na shoga wa mke wa Msungu ambao ndiyo wenye dili hizo.

Wanaamua sasa kuwa baada ya muda wanamteka mtoto kwa ajili ya kujipatia pesa.

Msungu haelewi ni kwa nini mtoto wake anatekwa, mkewe analifahamu hilo na mara kwa mara anawaonya Julio na shoga yake juu ya tabia hiyo, lakini wanatishia kutoa siri.

Mke wa Msungu mambo yakamtokea puani na sasa akawa hana amani ya ndoa. Muda wote mambo yanaweza kuharibika.

Anaamua kutafuta kundi ya wauaji kwa ajili ya kumuua Julio ili kunusuru ndoa. Hilo linafanyika.

Baada ya kuona Julio amefariki, shoga wa mke wa Stanley naye akaona yanaweza kumfika na yeye, akaamua kujiua mwenyewe. Hapo ndipo amani na furaha kwenye ndoa ya Msungu na mkewe ikapatikana



# HAKUNAGA TENA
## RIHANNA ATISHA KWA NOTI

BAADA ya kusuasua kwa miaka mingi kutokana na kuporomoka kimuziki, sasa mwimbaji nyota wa Marekani, Rihanna, ameibuka kwa kasi baada ya kutajwa kuwa anaongoza kwa utajiri kwa upande wa wanamuziki wa kike duniani.

Ripoti hiyo ambayo imemshtua hata Rihanna mwenyewe pia imewashangaza wengi baada ya mwanamuziki Beyonce ambaye alionekana kama kinara wa kukusanya pesa kutokana na kufanya matamasha kadhaa na mumewe Jay Z kutupwa kwa mbali.

Kulinagana na ripoti iliyotolewa na jarida la Fobes, Rihana ana utajiri unaofikia dola milioni 600 na kuwapita wakali wengine wengine kwa kuwa na kitita kikubwa cha fedha.

Fobes katika ripoti yake hivi karibuni inaeleza anayemkaribia Rihana ni Madonna ambaye amejikusanyia kitita cha dola milioni 570 na Celine Dion ameshika namba tatu akiwa na utajiri wa dola milioni 450.

Jambo la kushtua ni pale mke wa Yay Z, Beyonce ameshika namba tano kwa kuwa na ukwasi wa dola milioni 400 million.

Jarida hilo limesema kwamba, Rihanna amepata utajiri huo kupitia kazi zake za muziki, bidhaa za vipodozi, unamitindo na kipindi cha Sephora.

Pia Rihanna ameingia mkataba katika dili la kampuni ya LVMH kutangaza bidhaa zake za nguo, viatu na vifaa vingine vya urembo.

Kulingana na rekodi zilizopatikana idara ya mapato, Rihanna amepata dola milioni 570 kupitia biashara zake ndani ya mezi 15 pekee kuanzia mwaka jana

# Ufuoma jamani ndo nini kujianika



STAA wa filamu nchini Nigeria, Ufuoma Mcdermott, wiki hii ameibua gumzo katika mitandao ya kijamii baada ya kutupia picha akiwa na nguo aina ya bikini.

Ufuoma ambaye amejizolea wafuasi lukuki mitandaoni, aliweka picha hiyo katika akaunti yake ya Instagram na kusababisha mashabiki wake kumtolea povu kisawasawa.

Pamoja na kuambatanisha na ujumbe murua wa kimahaba, lakini hakuachwa hivihivi badala yake alianza kupewa lawama kutokana na kuvaa nguo hiyo ikiwa yeye ni mama wa watoto wawili.



## Nicolas, Erika talaka nje nje

NYOTA wa filamu nchini Marekani, Nicolas Cage, hatimaye ametangaza kuwa yupo singo baada ya kutalakiana na mkewe Erika Koike.

Cage na Erika walipeana talaka hivi karibuni baada ya mahakama ya Nevada kubaliki ndoa hiyo kuvunjwa kutokana na wawili hao kuwa na malengo tofauti.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Cage na Erika walitalakiana Ijumaa ya Mei 31,mbele ya jaji Clark County wa mahakama hiyo.

## Mercy unamtega Wizkid hivihivi

MKALI wa filamu kutoka Nollywood, Mercy Aigbe, ameamua kutoa ya moyoni baada ya kueleza angependa kukutana na wanamuziki Wizkid na Larry Gaaga.

Mrembo huyo amesema hayo kupitia ukurasa wake wa Instagram na kuelekeza kwamba nyimbo za wanamuziki hao zinamuaacha taabani pale anapozisikiliza.

"Wimbo unanipa hali mbaya!!! kila mmoja ananipa raha @larrygaaga au @wizkidayo wote wawili , ninasema kile ninachosema mtu mmoja alinipatia hawa watu,"





## Hongera Duncan kumleta mwana

MWANAMUZIKI mkali wa Nigeria, Duncan Mighty, amekuwa na furaha baada ya kupata mtoto wa tatu.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Mighty, alimkaribisha mtoto wake kwa kumpongeza mkewe Vivien Nwakanwa Mighty kujifungua kwa usalama.

"Mke wangu amejifungua, ungana name kumshukuru Mungu," aliandika pamoja na kulitaja jina la mtoto huyo kuwa anaitwa "Succeed Reign Mighty."

## Falz hujui radhi ya mama mbaya?

SIYO jambo la kawaida kusikia mzazi wa msanii mkubwa akilaumu mtoto wake kutokana kufanya makosa. Mama mzazi wa rapa Falz, yeye amekuwa tofauti baada ya kuonekana kukerwa na tabia ya mwanawe ya kutokwenda kanisani.

Kulingana na Falz mwenyewe wakati akihojiwa katika kituo kimoja cha televisheni, alisema mama yake huwa anamueleza jinsi anavyokosa raha kumuona mtoto wake akimuacha Mungu.

"Sina kitu chochote Kanisani, huwa siendi kusali jambo hilo mama linamfanya anilaumu na kunikemea," alisema.





**Na John Juma 0716217615**

## Mionzi ya Sheria

# Haki ya dhamana maana yake ni nini?

Ni kawaida kusikia mtu anakwenda katika kituo cha polisi , akiwa na mahitaji muhimu ya kisheria kumuwekea dhamana mtu wake wa karibu.

Ni mustakabali unaosababisha mtu kudodosa haja ya tafsiri neno dhamana na nafasi yake kisheria. Hapo ndipo inapofungua mlango katika kutolewa ufafanuzi wake, ndani ya mustakabali wake kisheria.

Inaelezwa kisheria, dhamana ni ruhusa ya uhuru anaoweza kupewa mtuhumiwa wakati ama uchunguzi wa kosa lake unaendelea au shauri lake likiendelea kusikilizwa mahakamani au akisubiri uamuzi wa rufani yake.

Hiyo ni haki inayopatikana kuptia msingi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambayo ina dhana inayotamka kwamba mtu hatochukuliwa kuwa mwenye hatia mpaka tuhuma zithibitishwe dhidi yake, kupitia Ibara ya13 (6) (b).

Ili kuzingatia dhana hiyo, ni muhimu kumruhusu mtuhumiwa kwa kumpa dhamana apate kuwa nje ya kizuizi mpaka hapo tuhuma zake zitakapothibitishwa na mahakama. Kwa mantiki hiyo, dhamana ni haki ya mtuhumiwa na wala sio upendeleo au zawadi.

Dhamana huweza kutolewa na jaji au hakimu, hali kadhalika, Mkuu wa Kituo cha Polisi ambako mtuhumiwa ameshikiliwa.

Hata hivyo, yapo baadhi ya makosa ambayo kisheria hayaruhusu dhamana, nayo ni: Mauaji ya kukusudia; uhaini; unyang'anyi wa kutumia silaha; ugaidi; sanjari na kosa la kunajisi; Kifungo cha 148(5) (a) (e) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985.

Hali kadhalika, mtuhumiwa anaweza kukosa dhamana kutokana na mazingira yafuatayo. Endapo:

Mtuhumiwa alishapewa dhamana akaikiuka; Kwa minajili ya usalama wa mtuhumiwa mwenyewe; usalama wa jamii; Kwa kuchelea kumwachia nafasi ya kuvuruga/kuharibu upelelezi; na sababu nyingine, yoyote ya msingi, kama atakavyoona Mkuu wa kituo.

Dhamana zipo za aina tofauti, na zenyewe ni kama vile: Dhamana ya mkataba wa Maandishi. Huo ni mkataba kati ya mtuhumiwa au mdhamini kujifunga kwamba mtuhumiwa atahudhuria Baraza la mahakama siku iliyotajwa. Iwapo mtuhumiwa asipotokea pasipo sababu muhimu, atalazimika kutekeleza masharti fulani au hata kifungo.

Dhamana ya Mali: Iwapo mtu hana kiasi cha fedha, anaweza kuweka dhamana kwa kukabidhi mali zake zinazohamishika.

Dhamana ya kutambuliwa: Aina hii ya dhamana humtaka mtuhumiwa au mdhamini kuweka sahihi ikiwa masharti ya mkataba wa dhamana yamevunjwa. Aina hii huonekana kama yenye unafuu kidogo.

Dhamana ya kuweka fedha: Hii ni aina ya dhamana ambapo, mtuhumiwa, rafiki au ndugu hutakiwa kutoa kiwango fulani cha fedha na iwapo hatahudhuria mahakamani fedha hiyo hutaifishwa na serikali.

Anayeweza kuomba dhamana? Mshitakiwa au rafiki wa mshitakiwa na wakili wa mshtakiwa.

Muda wowote wakati kesi inaendelea na wakati rufaa ikisubiriwa; Wakati mashitaka yanaandaliwa na polisi au kabla ya hukumu kutolewa au rufaa kuamuliwa.

Kifungu cha 67 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, mwaka 1985 kinaeleza kwamba, mtuhumiwa aliye chini ya ulinzi wa polisi anaweza kukataliwa maombi yake ya kutaka apewe dhamana.

Hii ni kwa kuzingatia masuala kama vile, polisi kujiridhisha kwamba mtuhumiwa atatimiza masharti ya dhamana atakayopewa, ikiwa kufika siku na saa atakayoamriwa.

Zaidi, kujua makazi, ndugu na jamaa, ajira na hata ikibidi hali ya maisha ya mtuhumiwa na familia yake, kumbukumbu za kihalifu kama zipo.

Baada ya mtuhumiwa kupewa dhamana ya polisi na kuwa huru dhamana hiyo inaweza kufutwa na mkuu wa kituo, chini ya Kifungu cha 68 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, mwaka 1985. Baadhi ya sababu zinazoweza kusababisha uamuzi wakufuta dhamana ni: Kubainika kwamba mtuhumiwa anapanga mipango kutoroka au makusudi anakiuka au yuko karibu kukiuka masharti ya dhamana

Adhabu kwa Kukiuka Masharti ya Dhamana; dhamana inayotolewa na polisi kwa mtuhumiwa anayekabiliwa na kosa la jinai inapaswa kuheshimiwa. Kifungu cha 69 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Mwaka 1985 kinaelekeza adhabu kali kwa mtuhumiwa na mdhamini au wadhamini wanapokiuka masharti ya dhamana waliopewa.

Dhamana inatolewa bure, hakuna malipo yoyote yanayotakiwa kutolewa ili mtuhumiwa au mshtakiwa akubaliwe dhamana.

Jambo la msingi ni mtuhumiwa kuomba apewe dhamana na kutimiza taratibu kwa mujibu wa sheria.

Ni muhimu mtuhumiwa kuwa nje kwa dhamana, ili aweze kujiandaa kukabiliana na tuhuma zinazomkabili kabla ya hajafikishwa mahakamani, mfano kupata msaada wa kisheria

Mwisho kabisa, dhamana ni haki ya kikatiba ya kila mtuhumiwa, kwa hiyo mtuhumiwa ana haki ya kuomba dhamana wakati wowote kabla hajapatikana na hatia au baada ya kukata rufaa kupinga hukumu iliyotolewa dhidi yake.

Pia dhamana ya polisi haihusishi fedha taslimu, hutolewa bure. Ni kosa kwa askari polisi kupokea fedha/rushwa katika zoezi la utoaji wa dhamana na katika utendaji kazi wake.



**Reubeni Lumbagala**

## Kalamu ya Mwalimu

# Tuzidishiwe uelewa wa kudhibiti mifuko plastiki

TANZANIA tunaweza tukiamua. Hivi ndivyo unavyoweza kusema ndugu msomaji wa safu hii. Ijumaa ya Mei31, 2019, ilikuwa mwisho ya kutumia mifuko ya plastiki nchini. Mwezi huu tulio nao, mifuko ya plastiki haikupaswa kutumika tena badala yake mifuko mbadala ichukue nafasi.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitoa kauli ya serikali kuhusu marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki. Tafiti zinaonyesha kuwa na madhara makubwa kwa ustawi wa mazingira na maisha ya viumbe hai.

Mnamo Aprili 9, mwaka huu alipokuwa akijibu hoja za wabunge katika mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Waziri Mkuu Majaliwa, anatamka:"Ifikapo Mei 31 mwaka huu itakuwa mwisho wa kutumia mifuko ya plastiki kubebea bidhaa mbalimbali. Kuanzia sasa tunatoa fursa ya viwanda kubadili teknolojia yao, wauzaji kuondoa mizigo yao na kumaliza kuuza yote na kadhalika."

Anaendelea kusisitiza: "Ofisi ya Waziri wa Nchi Makamu wa Rais itajiandaa kutumia kanuni chini ya Sheria ya Mazingira, ili kulifanya katazo hili kuwa na nguvu ya kisheria. Tunachukua hatua hii kulinda afya ya jamii, wanyama mazingira na miundombinu dhidi ya athari kubwa zinazotokana na taka za plastiki."

Nukuu hiyo ni sehemu ya mkazo uliotolewa na serikali kupitia Waziri Mkuu Majaliwa, kuhusiana na kuachana na matumizi ya mifuko plastiki, kuhamia mifuko mbadala ambayo ni rafiki kwa mazingira na maisha ya viumbe hai.

Mwanzoni, taarifa ya kuachana na matumizi ya mifuko ya plastiki ilionekana jambo gumu kutekelezeka kutokana na mazoea ya kutumia mifuko ya plastiki kwa matumizi mbalimbali.

Kutokana na msimamo thabiti wa serikali wa kuachana na matumizi ya mifuko ya plastiki na nchini, hivi sasa kuna mkazo wa kuongeza uzalishaji wa mifuko mbadala na suala hili sasa limekuwa halisi, yaani limewezekana.

Tanzania inaungana na Kenya na Rwanda kwa nchi za Afrika Mashariki na nchi nyingine duniani, ambazo zimeachana na matumizi ya mifuko ya plastiki.

Mifuko ya plastiki imekuwa na madhara makubwa kwa maisha ya viumbehai. Mathalani, mifugo inapoteza maisha kama itakula plastiki. Viumbehai wa baharini, pia vinapoteza maisha kwa kukosa hewa, pindi mifuko ya plastiki inapotupwa baharini.

Hivyo, juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi za kuinua sekta hiyo, zinaweza kushindwa kuzaa matunda ipasavyo kutokana na madhara ya plastiki kwa kusababisha vifo vya viumbe hai hivyo.

Aidha, mifuko hiyo ya plastiki imekuwa na madhara pia kwa mazingira. Mifuko hiyo imekuwa chanzo kikubwa cha kusababisha kushindikana kuozesha taka kwenye vituo vya kukusanyia taka.

Taka zinazotupwa katika mashimo na vituo vingine vya kukusanyia taka zimekuwa zikidumu kwa muda mrefu kutokana na mifuko ya plastiki kuwa na uwezo wa kukaa kwa muda mrefu bila kuoza.

Ni jambo linalosababisha kuendelea kudumu kwa taka na kuchafua kwa kiasi kikubwa mazingira yetu. Athari nyingine zipo katika miundombinu, mifuko ya plastiki imekuwa ikisababisha kuziba kwa mifereji, hali inayochangia mafuriko, kwani maji yanashindwa kupita katika mifereji.

Mifuko ya plastiki imekuwa chanzo kikubwa cha kuzuia maji kushindwa kupita katika mifereji, hivyo inasababisha kutokea kwa mafuriko kila ifikapo majira ya masika.

Kutokana na hali hiyo, kuna uharibifu wa miundombinu kama madaraja na barabara unaotokea katika kipindi cha mvua. Ijulikane, miundombinu ni moja ya maeneo yanayotumia fedha katika ujenzi na ukarabati wa miradi yake.

Hivyo, ni lazima wananchi wafahamu namna mifuko ya plastiki imesababisha hasara kubwa kwa sekta ya miundombinu, kutokana na mifuko ya plastiki kusababisha mifereji na mitaro kuziba, hatimaye kutokea mafuriko yanayoathiri miundombinu.

Niseme, mifuko mbadala ni mwelekeo mzuri wa kuokoa fedha nyingi, zilizokuwa zikikarabati miundombinu, kutokana na madhara ya mafuriko.

Pamoja na kwamba tumeshaanza kutumia mifuko mbadala, upo umuhimu wa kuendelea kutoa elimu zaidi kuhusiana na athari za mifuko ya plastiki na umuhimu wa matumizi yake kwa maendeleo yetu.

Serikali nayo inapaswa ishirikishe sekta binafsi katika kutoa elimu hii, ili kujenga jamii ya watu wenye uelewa. Vyombo vya habari navyo vitumike kwa juhudia kuielimisha jamii.

Wananchi waone matumizi ya mifuko mbadala ni mkombozi kwa maisha yao wenyewe na si kwa faida ya serikali. Watoe ushirikiano wa kutosha katika kutumia mifuko mbadala ambayo ni rafiki wa mazingira na afya zetu.

Cha muhimu, wawekezaji zaidi wajitokeze kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa, ili bidhaa ya mifuko mbadala zipatikane kwa bei rafiki ambayo wananchi wa wafanyabiashara wataimudu. Tafakari.

- **Mwandishi wa makala hii ni mwalimu katika Shule ya Sekondari Mlali, iliyopo wilaya ya Kongwa, Dodoma. Anapatikana kwa simu: (+255) 764 666349.**

## RASHARASHA KIGODA CHA MWALIMU...

# Mijadala kubadili mfumo wa elimu inavyodai serikali kuchukua hatua

**Na Beatrice Moses**

WASOMI kadhaa wanatamani mfumo wa elimu ufumuliwe na kusukwe upya, kwa lengo la kuwezesha kupatikana wahitimu wengi wenye uwezo wa kujiajiri na wanaoleta ushindani katika soko la ajira.

Wakichangia kuhusu mfumo wa elimu nchini na Afrika wakati wa mjadala kwenye Tamasha la 11 la Kigoda cha Mwalimu Nyerere, wamebainisha kuwa elimu inayotolewa sasa haikidhi mahitaji yaliyopo, hivyo kusababisha pengo, hasa kwenye sekta ya ajira.

Dk. Evalisto Mtitu, ni Mhadhiri wa Mitaala ya Elimu kutoka Chuo Kikuu Huria(OUT), anasema mjadala huo unasaidia kupata namna nzuri ya kuboresha elimu nchini na Afrika kwa ujumla.

Anasema, katika Karne ya tuliyopo wanataaluma wanapaswa kuwaandaa wanafunzi wajitegemee na kuendeleza falsafa ya Mwalimu Nyerere, kuunganisha nadharia na vitendo, ili kumwezesha anayepata elimu ajitegemee katika kujitafutia kipato.

"Aina ya ufundishaji uliopo, wanafunzi wanafundishwa kwa mbinu za zamani ya nadharia zaidi ambayo haiwezi kusaidia wakihitimu waweze kujiajiri, ufundishaji unaolenga zaidi mitihani lakini siyo vitendo," anasema Dk Mtitu.

Anasema, ni hali inayochangia uwepo vijana wengi wahitimu mtaani na Dk. Mtitu anafafanua: "Mwanafunzi anapata elimu ya kujibu mitihani yaani wafaulu kwa alama za juu na siyo kuwa na mbinu za kuyakabili maisha, hivyo atakumbuka ili kukidhi matakwa ya walimu au taifa anapopimwa kwenye mitihani ya taifa."

Anasema aina ya ufundishaji uliopo umejikita kwenye kuwaandaa wanafunzi kupata maksi za juu zaidi.

### MKURUGENZI KALLAGE

Mkurugenzi wa Haki Elimu, John Kallage, anasema mfumo wa elimu nchini haukidhi, kwani haujawafanya wahitimu kuanzisha vyanzo vya mapato au kushindana kwenye soko la ajira.

"Ili kupata maendeleo suala la elimu ni ufunguo mada zilizowasilishwa mfumo wa elimu haulingani na mahitaji ya sasa, hivyo kuna umuhimu wa kuwa na mjadala mpana kuhusu jambo hili," anasema.

"Tunapaswa kuangalia tatizo kubwa lipo wapi namna gani tunaweza kutoka hapo, tuchukue hatua za kuboresha mfumo wetu wa elimu. Hivyo, mjadala huu ni sehemu ya mjadala tunaoutaka wa kitaifa kuhusu namna gani elimu inayotolewa iweze kwenda na matakwa ya sasa," anasema




Mtoa mada, Profesa Patrick Lumumba kutoka nchini Kenya, akiwa katika Tamasha la 11 la Kigoda cha Mwalimu Nyerere hivi karibuni kwenye ukumbi wa Nkurumah, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: BEATRICE MOSES**

Kallage anasema, kuna mapendekezo yatatolewa ambayo yanaweza kutoa mchango katika kutafuta suluhisho kwa jambo hilo. Majadiliano yanalenga kuangalia elimu katika ngazi zote, kuanzia shule za mingi na sekondari, vyuo vikuu na vyuo vya ufundi.

### KUPANDISHA ELIMU

Mhadhiri wa Saikolojia ya Elimu na Taaluma za Mitaala kutoka Chuo cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Dk. Florence Kyaruzi, anasema inabidi kufanyike tathimini katika hatua za kuboresha tunapata changamoto na pia tunapata mrejesho.

Dk. Abdallah Hamza wa UDSM, anabainisha kuwapo tatizo la baadhi ya jamii kutoona umuhimu wa elimu kwa watoto wao, kwamba kupitia utafiti uliofanyika Ilula Iringa, ulibaini watoto wenye umri kati ya miaka sita na 17 wako shambani.

Anasema, asilimia 81 ya wazazi wanakubaliana katika eneo la Buhemba, Mara, utafiti ulibaini watoto wameajiriwa kwenye kampuni kubwa na ndogo za migodi kinyume na sheria za nchi ambapo haziruhusu ajira kwa watoto.

Mwenyekiti wa Kigoda cha Mwalimu, Profesa Rwekaza Mukandala, katika maoni yake anasema tamasha hilo pamoja na mijadala yake, wamekusudia kujadili nafasi ya elimu na ubora wake na jinsi namna inaweza kuleta maendeleo.

Anasema, Aprili mwaka huu kwenye mafunzo ya namna ya kuendeleza kuwajengea uwezo wadau, wana mkakati wa kukuza stadi za kazi na ujuzi (ESPJ), uliibuka mjadala wa namna gani kasi ndogo ya kuzalisha wajuzi inavyochelewesha maendeleo nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania(TPSF), Godfrey Simbeye, anasema kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi,Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, taasisi imetekekeza mkakati wa Taifa kuendeleza ujuzi, kupitia mradi wa kukuza stadi za kazi na ujuzi.

Anabainisha kuwa TPSF iliandaa mafunzo hayo kwa wadau ili kutoa ufahamu na maendeleo juu ya mabaraza ya ujuzitangu kuanzishwa kwake.

Mabaraza hayo yameanzishwa na TPSF, pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, yanatarajiwa kutumika katika kuibua, kukuza na kuendeleza ujuzi katika sekta kadhaa kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Simbeye anasema, sekta sita zimepewa kipaumbele katika jukumu la kuanzishwa mabaraza ya ujuzi wa kisekta kwa maendeleo ya nchi.

Anazitaja sekta hizo kuwa ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Kilimo, Uchukuzi, Utalii, Ujenzi na Nishati.

Mshauri Mwelekezi, Nicholous Mbwanji, anabainisha kuwa nchi nyingi za uchumi wa kati zimejikita katika kuhakikisha idadi ya wenye ujuzi inazidi kupaa hata hivyo kwa Tanzania hali imekuwa tofauti.

"Wakati nchi hizo zinahakikisha kuwa zinaongeza idadi ya msomi mmoja wa elimu ya juu, mafundi wajuzi watatu, Tanzania imejikita kuongeza wasomi wengi badala ya wajuzi," anasema Mbwanji na kushauri mfumo wa elimu kuhakikisha unazalisha wajuzi wengi zaidi, badala ya wasomi wenye vyeti wasiokuwa na ujuzi.

"Ifike wakati tujiulize mtu analipwa mshahara mkubwa kwa ujuzi au cheti cha usomi wake, hii imesababisha wajuzi kuwa na mishahara midogo hivyo nao kuamua kuweka ujuzi pembeni ili kwenda kusaka vyeti vya elimu ya juu," anasema

Washiriki kadhaa katika mafunzo hayo walishauri serikali kuweka mfumo mzuri katika elimu ya ufundi, ili kuruhusu waendelee na elimu hiyo kwa ngazi tofauti ikiwezekana hadi uprofesa wa ujuzi kulingana na ufundi anaosomea.



Baadhi ya viongozi kwenye Tamasha la 11 la Kigoda cha Mwalimu Nyerere, lililojadili mustakabali wa elimu barani Afrika.

MAKALA

# Azimio la Arusha muhimu zaidi sasa kuliko enzi zile

**Na Moses Ismail**

MOJA ya mambo yanayowapa faraja Watanzania ni kuona serikali inatimiza miradi mingi ya maendeleo kwa fedha za ndani na inakuwapo misaada au mikopo, ni ile isiyoumiza, kama ilivyoshuhudiwa katika zama za uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere.

Katika kuhimiza hilo jana, Rais John Magufuli, alikutana na umma, wadau mbalimbali kitaifa, kupata maoni kuhusiana na mwenendo wa biashara na uchumi nchini.

Hivi sasa inashuhudiwa serikali ikitekeleza miradi mikubwa kama vile ujenzi wa reli ya kisasa, SGR, kuimarisha shirika la ndege nchini, ATCL, uzalishaji umeme mradi wa Stigler's Gorge na ujenzi wa vituo vya afya 208.

Katika zama za uongozi wa Mwalimu Nyerere, miradi kama hiyo ilifanyika kuongeza chachu ya maendeleo kitaifa. Hapo inakumbukwa ujenzi wa reli ya Tanzania na Zambia (Tazara), Mradi wa Umeme wa Maji Kihansi.

Pia, kuna kuimarishwa Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA) na Shirika la Ndege la Tanzania (ATC), baada ya kuvunjika iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwaka 1977.

Katika hatua ya kwanza, serikali ilisimamia uchumi nchini katika mfumo hodhi. Katika hatua ya kwanza, baada ya miaka mitatu ya uhuru, hadi kufikia mwaka 1985 ilikuwa sera hodhi ya kiuchumi.

Hapo iligusa njia kuu za uchumi katika kudhibiti na kusimamia sekta za uchumi, uzalishaji na biashara, fedha ikiwamo benki, kwa kutambua kote huko ni muhimu na ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi.

Ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Sasa ni miaka 34 ya mabadiliko katika mfumo wa uendeshaji uchumi kitaifa.

Pia, Mwalimu Nyerere anakumbukwa alivyokuwa makini katika kudhibiti sekta kuu mbili; mafuta na fedha za kigeni. Alifanikiwa kustawisha uchumi wake na kutoa huduma za kijamii, kabla ya balaa la Vita ya Uganda.

Lingine la kuhujumu uchumi, lilifuatia baada ya vita kutikisa na kuvunja nguvu mfumo mzima wa uchumi wa serikali.

Suala la uhujumu uchumi nalo lilikuwa vita nyingine vilivyoendeshwa na nguvu za fedha na mipango ya kibeberu, baadhi ya watu kujilimbikizia mali kinyume na utaratibu na kisheria na sera wakati huo .

Mbinu kubwa iliyotumiwa ni watu kuhujumu pato la kodi ya serikali, ikiwamo 'kufunga bomba' la mtiririko wa kodi inayostawisha pato la serikali, ikiwamo bidhaa zinazonunuliwa moja kwa moja toka viwandani.

Kuna wahujumu uchumi wa wakati, baadhi walibuni mtindo wa kununua bidhaa kutoka viwanda na wakazificha kwenye maghala yao, ili kudhibiti mzunguko wa fedha.

Ilibainika kwamba, walikuwa na malengo mawili makuu: Mosi, kuhakikisha serikali ambayo ilitoka katika vita vya mwaka mmoja na nusu, inatetereka kiuchumi na haitaweza kutimiza lengo lake la kufufua uchumi kupitia rai ya wananchi 'kufunga mikanda.'

Pili, lengo lingine la wahujumu uchumi ni kujenga chuki ya wananchi serikali. Yapo madhara yalishuhudiwa kupitia upungufu huo.



Mwalimu Julius Nyerere, alipokuwa katika matembezi ya Azimio la Arusha. **PICHA: MTANDAO**


Wakati wote huo, Azimio la Arusha Mwaka 1967, ndicho kikawa chombo mahsusi kukabili mambo yote muhimu ya kuhakikisha sera na sheria zote zinafuatwa.

Inasikitisha kwamba, katika kipindi cha mpito kuelekea sera za uchumi huria na kuruhusu viongozi wa serikali kumiliki mali, imeshuhudiwa miiko hiyo ambayo hadi sasa ina uhai, lakini baadhi ya wasio wema katika nafasi mbalimbali hawatekelezi, hata viongozi husika wanaonyesha kiburi.

Ni aina ya kiburi ambacho hadi sasa Rais Dk. John Magufuli, amekuwa akiingilia kati kuzima kiburi husika. Hapo ndipo inapoonyesha haja ya kurejea Azimio la Arusha, katika namna yoyote, maana linahitajika kukabili yaliyoko sasa.

Pia, ndio inasaidia kuihuisha hata masuala kama ya kuhakiki mali za viongozi, kabla ya kuingia madarakani na baada ya hapo.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 4 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Mlima mrefu duniani
5. kitu cha thamani
7. Mji mkuu wa Marekani
10.Watu wa New Zealand
12.Mkuu wa Jamhuri
13.kata shauri 14. sahihi
15.Tia kisu makali 16.Keti
18.Uwazi mwembamba ukutani
19.Wanyanganyi 20. tundu
22.toa makosa 26.Konde
27.Mji mkuu wa Kolombia
28.Ndugu wa kiume wa baba
29.Mkutano wa kikundi cha kujifunza kitu fulani

**Dondoo: Chini**

1. Aligombea Urais UKAWA
2. mionzi inayoonyesha vya ndani 3. Lome ni mji mkuu
4. madini ya metali
5. tembea kwa kufuatana
8. Shika kitu mtegoni
9. Garimoshi
11.Ottawa ni mji wake mkuu
16. Kitu chenye uhai
17.matokeo baada ya tukio
18.hali ya kuota kwa mmea
21.choma juujuu bila ya kuiva
23.Fuatisha mtu
24.Nyumba
25.Ubinadamu

**Jibu Na: 3**

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | L | G | E | R | I | A | ■ | A | ■ | U | ■ | T |
| L | ■ | H | ■ | ■ | ■ | N | I | G | E | R | I | A |
| A | D | O | W | A | ■ | D | A | U | ■ | A | ■ | N |
| S | ■ | R | ■ | N | ■ | A | S | A | D | I | ■ | G |
| K | I | O | N | G | O | Z | I | ■ | H | A | B | A |
| A | ■ | F | ■ | A | ■ | I | ■ | ■ | A | ■ | ■ | N |
| ■ | K | A | I | M | U | ■ | D | U | M | A | ■ | Y |
| ■ | W | ■ | S | I | M | B | A | ■ | B | ■ | ■ | I |
| M | A | S | I | Z | I | ■ | H | ■ | I | R | A | K |
| ■ | N | ■ | K | A | Z | O | O | ■ | ■ | A | L | A |
| M | Z | E | E | ■ | A | ■ | M | A | L | T | A | ■ |
| ■ | A | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | E | ■ | O | A | M | A |
| ■ | ■ | K | U | K | A | N | Y | W | A | ■ | A | ■ |




Wananchi wakiwa katika shughuli ya kupima maambukizi ya HIV, moja ya magonjwa yanayoambukizwa kupitia zinaa. **PICHA: MTANDAO**

# WHO: Maambukizi ya magonjwa ya zinaa sasa ni milioni moja kwa siku

KIWANGO cha kimataifa cha maambukizi ya magonjwa ya zinaa (STI) kwa hivi sasa kinapaswa kuwa kengele ya kuziamsha serikali mbalimbali duniani.

Hilo ni onyo ambalo linatolewa na wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN) wa masuala ya afya, wakibainisha takwimu za maambukizi mapya ya magonjwa hayo kwa hivi sasa.

Wataalamu hao wanaweka wazi kwamba kiwango cha maambukizi kinaonyesha kuwa mtu mmoja kati ya 25 anaambukizwa kila siku na moja ya maradhi ya zinaa yanayotibika.

Aidha, wanasema kwamba kwa ujumla kuna maambukizi ya zaidi ya watu milioni moja kwa siku ya magonjwa ya zinaa.

Kutokana na madhira hayo, Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) linaeleza wasiwasi wake hasa kutokana na kukosekana kwa hatua madhubuti za nchi mbalimbali kukomesha kusambaa kwa maambukizi ya magonjwa hayo na mengine ya zinaa.

WHO inaonya kwamba endapo maradhi hayo yataachwa bila kutibiwa yanaweza kuwa na athari kubwa katika afya hasa ya barubaru, watu wazima na watoto ambao hawajazaliwa. Akisisitiza umuhimu wa kuchukua hatua sasa, Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma ya Afya kwa wote wa WHO, Dk. Peter Salama anasema: "Hii ni kengele ya kuziamsha pande zote husika katika kuchukua hatua za pamoja ili kuhakikisha kila mtu, kila mahali anaweza kupata huduma anazohitaji katika kuzuia na kutibu magonjwa haya za zinaa."

**ATHARI ZA MAGONJWA YA ZINAA**

Kwa mujibu wa ripoti ya WHO ya wataalam hao, athari mbaya za magonjwa manne mashuhuri ya zinaa yanayotibika ambayo ni klamidia, kisosonono, kaswende na muwasho sehemu za siri ni pamoja na athari za mishipa na magonjwa ya moyo. Lakini kutozaa, kupoteza ujauzito, matatizo wakati wa ujauzito, watoto kufia tumboni na ongezeko la hatari ya kuambukizwa ukimwi, HIV. Kwa upande wake, Dk. Melanie Taylor, mtaalamu wa masuala ya kisaikolojia wa WHO katika idara ya afya ya uzazi na utafiti anasema: "Kwa wastani takwimu hizo zinaonyesha kuwa mtu mmoja kati ya 25 duniani kote angalau ana aina moja ya magonjwa ya zinaa yanayotibika huku wengine wakiambukizwa zaidi ugonjwa mmoja kwa wakati mmoja,"

Anaongeza: "Na hivyo kuibebesha dunia mzigo mkubwa wa STI... WHO mara ya mwisho ilichapisha takwimu za magonjwa ya zinaa mwaka 2012 na hadi sasa maambukizi ya magonjwa hayo hayajapungua sana."

**WAATHIRIKA WAKUBWA**

Matokeo ya utafiti wa kimataifa wa WHO kwa mwaka 2016 umeonyesha kwamba kwa wanawake na wanaume wa umri wa miaka kati ya 15 hadi 49 kuna maambukizi zaidi ya milioni 376.

Unafafanua kwamba katika maambukizi hayo, ugonjwa wa muwasho unaongoza kwa visa milioni 156, ukifuatiwa na klamidia visa milioni 127, huku kisonono kikiwa na visa milioni 87 na kaswende visa milioni 6.3.

Unabainishwa kwa ujumla kwamba magonjwa hayo kwa mwaka 2016 yalisababisha watoto takribani 200,000 kufia tumboni.

Aidha yalisababisha idadi kubwa ya vifo vya watoto wachanga na kufanya kuwa sababu iliyoongoza kwa vifo vya Watoto duniani kwa mwaka huo.

Ingawa WHO inasema magonjwa haya yanaweza kutibika na aina mbalimbali za dawa zilizopo, linaonya kwamba upungufu mkubwa duniani kote wa hivi karibuni wa dawa aina za benzathine penicillin umefanya kuwa changamoto kutibu ugonjwa wa kaswende.

Pia ripoti inasema usugu wa viuvijasumu dhidi ya ugonjwa wa kisonono nao umekuwa ni moja ya tishio la kiafya linaloongezeka na huenda ukasababisha kuwa vigumu kutibu ugonjwa huo

Kwa ujumla bakteria zaidi ya aina 30, virusi na wadudu wengine wanajulikana kuambukizwa kupitia ngono isiyo salama.

Lakini pia maradhi mengine yanaweza kuambukizwa kwa kupewa damu iliyoambukizwa pamoja na kutumia sindano zisizo salama hasa miongoni mwa watumiaji wa mihadarati.

**MARADHI YASIYOTIBIKA**

Mbali ya magonjwa haya manne yaliyotajwa kwenye ripoti ambayo yanatibika, aina zingine nne ni za virusi visivyotibika ambavyo ni homa ya ini aina B, virusi vya malengelenge aina 1 na 2 au HSV, virusi vya HIV na HPV.

Pia shirika hilo linasema magonjwa mengi ya zinaa yanaweza kuambukizwa kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito au kujifungua ikiwamo klamidia, kisonono, homa ya ini aina B, HIV na kaswende.

Kwa mantiki hiyo WHO inasema upimaji kwa wakati na matibabu ni muhimu sana katika kupunguza mzigo wa magonjwa hayo ya zinaa kimataifa. Aidha, shirika hilo limetoa wito kwa kina mama wajawazito kufanyiwa uchunguzi wa mara kwa mara hasa kwa maradhi ya kaswende na HIV.

**KWA MUJIBU WA TAARIFA YA UN**

HABARI KIMATAIFA

# Waziri Mkuu Ethiopia ajitosa mgogoro Sudan

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, yupo mjini Khartoum kuanzia jana, kujaribu kuwapatanisha watawala wa kijeshi na makundi ya upinzani.

Viongozi wa makundi yanayopigania uhuru na mabadiliko na yanayotaka demokrasia nchini humo yamekataa mazungumzo zaidi na yametoa wito wa kuvunjwa kwa kikosi cha uingiliaji kati cha wanamgambo cha Rapid Support Forces ambacho wanakishuhtumu kuwaua mamia ya watu.

Wapinzani hao walisema kuwa jeshi lazima likabidhi mamlaka mara moja kwa mamlaka ya kiraia ya mpito.

Kwa miezi kadhaa sasa, baraza la utawala wa mpito la kijeshi nchini Sudan limekuwa na utashi wa kuwa na ushirikiana na mataifa mengine.

Lakini, kutokana na taarifa za mauaji ya waandamaji Jumatatu wiki hii na kuendelea kwa mateso na vitisho dhidi ya raia kumekuwa na kauli za kulaani dhidi ya utawala wa mpito wa kijeshi.

Muungano wa Afrika tayari umekwishatoa wito wa kufanyika kwa uchunguzi juu ya mauaji ya hivi karibuni na imetishia kuwawekea vitisho maofisa binafsi wanaokwamisha mchakato wa kipindi cha mpito kuelekea demokrasia.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed anaangaliwa kama mwana mageuzi na alikwishakutana na baraza la jeshi hilo hapo awali.

Hata hivyo , utatakiwa kuwapo ushawishi mkubwa katika mchakato huo na makubalino na majenerali ili kuweza kuanzishwa kwa mazungumzo mapya ya uundwaji wa serikali ya kiraia.

Muungano huo wa Afrika umetaka uchunguzi kufanywa kuhusu mauaji hayo ambayo yanadaiwa kutekelezwa na vikosi vya usalama.

Tume ya Afrika hiyo inasema kuwa marufuku hiyo ilikubaliwa na wanachama na itaanza kutekelezwa mara moja.

Wiki hii Tume ya Amani na Usalama katika Umoja wa Afrika ilisema kuwa ilichukua uamuzi huo kufuatia mauaji ya raia wasio na hatia nchini Sudan katika kipindi cha siku tatu zilizopita.

Vilevile ilisema imetishia kuchukua hatua dhidi ya watu binafsi katika baraza hilo la mpito iwapo jeshi litakataa kukabidhi mamlaka kwa raia.

Muungano huo umetaka uchunguzi kufanywa kuhusu mauaji hayo ambayo yanadaiwa kutekelezwa na vikosi vya usalama.

*BBC*



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, akizungumza na wadau wa serikali ya mpito huko Sudan. **PICHA: MTANDAO.**

# Rais Mutharika ahofia kupinduliwa

**BLANTYRE, Malawi**

RAIS wa Malawi, Peter Mutharika, ameutuhumu upinzani nchini humo ambao umekataa kutambua ushindi wake katika uchaguzi wa mwezi Mei mwaka huu, kwa kutaka kuipindua serikali yake kwa nguvu.

Rais Mutharika anadai kuwa Lazarus Chakwera, kiongozi mkuu wa upinzani na wafuasi wake wanapanga njama kuipindua serikali yake, wakati huu watu wanaounga mkono upinzani wakidai kiongozi wao aliibiwa kura.

Katika hatua nyingine, Balozi wa Marekani nchini Malawi Virginia Palmer, alilazimika kukimbia siku ya Alhamisi wiki hii kutoka katika makao makuu ya chama cha upinzani cha Malawi Congress Party jijini Lilongwe baada ya polisi kurusha mabomu ya kutoa machozi.

Balozi Palmer, alisema alikuwa amekwenda kumuaga kiongozi wa upinzani kabla ya kurejea nchini Marekani kwa sababu muda wake wa kuhudumu nchini Malawi, unafika mwisho wakati alipokabiliana na hali hiyo.

Chakwera ambaye alishindwa na rais Mutharika kwa kura karibu 190,000 alisema hawezi kukubali na kumtambua mpinzani wake kama rais na ataendelea kushinikiza haki kutendeka.

Tayari amewasilisha kesi mahakamani kupinga ushindi wa rais Mutharika ambayo ilimpa ushindi na sasa anaongoza serikali.

Peter Mutharika alishinda uchaguzi wa Malawi kwa mara ya kwanza miaka mitano iliyopita na kumuondoa madarakani rais wa kwanza mwanamke nchini humo Joyce Banda.

Kiongozi wa chama cha upinzani cha Democratic Progressive nchini Malawi, Peter Mutharika, aliahidi kuwa kazi yake kubwa itakuwa kuwaunganisha Wamalawi baada ya mvutano wa muda mrefu katika maswala ya uchaguzi.

Alitoa wito kwa washindani wake kuungana naye katika kujenga taifa hilo changa lililoko kusini mwa Afrika

*RFI*

## Theresa May ang'atuka rasmi Conservative

**LONDON, Uingereza**

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Theresa May, ameng'atuka uongozi wa chama tawala cha Conservative rasmi jana, hatua inayofungua mlango wa kinyang'anyiro cha mrithi wa nafasi hiyo.

May hatauhutubia umma lakini anatarajiwa kuwasilisha barua ya kuthibitisha kujiuzulu kwake kwa kamati ya chama chake yenye nguvu ijulikanayo kama "Kamati ya 1922".

May ataendelea kuwa Waziri Mkuu hadi wabunge watakapomchagua kiongozi mpya wa chama hicho mchakato utakaouchukua hadi miezi miwili.

Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Boris Johnson anapewa nafasi kubwa ya kushinda nafasi hiyo. Waziri Mkuu May alitangaza kujiuzulu nafasi hiyo Mei 24 mwaka huu baada ya kushindwa kufanikisha makubaliano ya Uingereza kujiondoa Umoja wa Ulaya maarufu kama Brexit

*DW*

## WHO yaonya ongezeko magonjwa ya ngono

**GENEVA, Uswisi**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeelezea wasiwasi kuhusu kukosekana kwa hatua za kukabiliana na magonjwa yanayosambazwa kwa ngono.

Wakati hayo yakitokea mmoja wa wataalamu wake ameonya kuhusu mitandao ya kukutanisha wapenzi kuwa ndiyo inayochangia kuchochea kuongezeka kwa maambukizi hayo.

Katika ripoti mpya ya shirika hilo, taarifa ilisema kuwa zaidi ya watu 1,000,000 wanaambukizwa magonjwa ya ngono kila siku duniani.

Kwa mujibu wa WHO mwaka 2016 zilitolewa taarfa za visa vipya milioni 376 vya magonjwa ya chlamydia, kisonono, trichomoniasis na kaswende duniani kote sawa na rekodi iliyopita ile ya mwaka 2012 ikiwa ni idadi kubwa zaidi.

Mtaalamu wa magonjwa hayo wa WHO, Theodore Wi aliwaambia waandishi wa habari kuhusiana na wasiwasi wa kupungua kwa matumizi ya mipira ya kujikinga na magonjwa ya ngono 'kondom' kwa kuwa watu wamepoteza hofu ya kuambukizwa Ukimwi kufuatia hatua zilizofikiwa na upatikanaji wa dawa za kufifisha makali ya Virusi vya Ukimwi (VVU) za ARVs.

*DW*

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.

Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# Jumba Jekundu-4

**Na Adam Fungamwango,**

**(0716 350534)**

"Unajua Kadili, mimi ndiyo mama yako, nimekuweka kwenye tumbo hili, miezi tisa, nimekuzaa, nimekunyonyesha, nimekuogesha, najua kila kitu juu yako, uwe na furaha, uwe na huzuni, wewe kuna kitu kinakutatiza, ila hutaki kusema." Alisema akimuangalia mwanaye kwa macho makali ya kumsuta kuwa ni kweli anachoongea.

Kadili aliondoa macho yake kukutana na ya mama yake kwa sababu aliona kama vile yamepenya kabisa ndani ya moyo wake na kukutana na ukweli wenyewe.

Ni kweli hayuko sawa. Picha ya binti mrembo asiyemjua jina ilimjia. Picha ya kukumbatiwa na mrembo ambaye uzuri wake hajapata kuuona kwenye maisha yake, wala tu kudhani kuwa anaweza kutazamwa na msichana wa aina hiyo, achilia mbali kuombwa kucheza naye, ilimtatiza.

Kila dakika zilivyozidi kwenda mbele, ndipo mawazo yalipozidi kumjaa kichwani. Kwanza alijiona ni mtu mwenye bahati kubwa kuliko mwanaume mwingine yoyote yule usiku ule ndani ya ukumbi wa Blue Star.

Hakuwa na uhakika kuwa binti yule alifanya vile kwa sababu anampenda au kwa sababu alicheza vizuri.

Hata hivyo aliondoa mawazo kuwa binti yule amempenda kwa sababu jinsi alivyo alionekana ametoka kwenye maisha ya juu, kutokana na mavazi na kila kitu kilichopo mwilini mwake, huku yeye akiwa ametinga mavazi ya kawaida ambayo hayakuwavutia watu wengi mle ndani. Mchanganyiko ule wa mawazo, ndiyo yaliyomfanya kutokuwa kwenye hali yake ya kawaida kiasi cha mama yake kubaini hilo.

"Haya kama huna sawa, lakini mimi naona lipo, na kama lipo mimi nitajua tu, mimi ndiyo mama yako hakuna mwingine ujue." Alimtahadharisha. Kadili akaitikia kwa kichwa.

****************************************

Anaitwa mama Gombea. Zamani wakati wa usichana wake aliitwa Mwajabu. Alizaliwa Chalinze mkoani Pwani. Hakuona umuhimu wa shule. Alikuwa akienda kutimiza wajibu. Mwalimu akiongea yeye linapita sikio hili na kutokea sikio lingine. Alipofika darasa la nne akajionea tabu, akaamua kujiachia na shule yenyewe.

Kazi yake ikawa kupika vitumbua na kuuza kwenye barabara kuu itokayo Dar es Salaam kwenda Morogoro. Akampata dereva mmoja wa malori na kumdanganya kuwa atamuoa, hivyo atoroke waende naye Dar. Bahati iliyoje. Alikuwa hajawahi kufika. Alikuwa




anaisikia tu.

Alipofika jiji lilimpokea. Kama kawaida ya Dar ni jiji la furaha na karaha. Badala ya kuolewa akafanywa nyumba ndogo. Akapangishiwa chumba maeneo ya Tandale kwa Mtogole. Mbali na kuwa na mke wa ndoa, bwana wa mama Gombea alikuwa pia na wanawake kibao si hapa Dar tu, bali hata huko mikoani anakopita na malori anayoendesha.

Pamoja na kuona amedanganywa, Mwajabu hakuona kabisa umuhimu wa kurudi kwao Chalinze. Japo aliishi maisha ya hali ya chini, lakini aliyaona ni mara kumi zaidi kuliko yale ya Chalinze.

Kwanza kabisa alikuwa analipiwa chumba na sebule na bwana yake. Kazi ya kuuza vitumbua aliyokuwa akiifanya kwao, aliihamishia Dar, hivyo alikuwa akipata visenti viwili vitatu vya kununulia nguo, vipodozi na kucheza michezo ya upatu na akinamama wenzake.

Bwana yake pia alikuwa akimtupia visenti vya kuweza kukidhi mahitaji, kiasi kwamba aliweza kumuda maisha ya mjini. Alipata pesa zake za mchezo, baadhi anazituma kwa wazazi wake, huku zilizobaki anamalizia shida zake.

Pamoja na yote hayo, sifa kubwa ya mama Gombea ambaye kwa sasa tayari ana watoto watatu, ni umbea.

Hakuna kinachompita mtaani. Chochote kile ataanza kukijua yeye kabla ya yoyote yule. Alikuwa akisambaza habari yoyote ile ambayo hakuna ambaye ameanza kuisikia, au hata kama kuna watu wameanza kuisikia ni wachache sana.

Hakuwa analipwa chochote kwa kazi hiyo, faraja yake ni kuona anapata taarifa na kuzisambaza kabla watu kuijua.

Siku hiyo alikuwa amefika mapema asubuhi, kiasi cha saa mbili hivi nyumbani kwa mama Kadili.

"Mwali wee bado umelala mwenzetu." "Hapana mama Gombea, nabandika chai." Mama Kadili alijibu

"Haya wageni ndiyo tumekuja hivyo, uongeze mikate." Mama Gombea alijikaribisha.

"Mikate wapi mwenzangu, nimechemsha ndizi." Alisema Mama Kadili huku akiwa ametoka nje kwa heshima ya jirani yake.

"Enhee tena umenifikisha mahala pake."

"Basi karibu, ngoja nikuletee kigoda."

"Ngoja nikae kidogo tu nitie baraka, nimepita tu hapa naenda huko kwa mama Mtupeni kumtaarifu shughuli ya mpwa wangu Sheila."

"Lini tena."

"Mwezi ujao mwishoni, sare bado sijatafuta, niliipata na wewe nitakuletea, unajua wewe mwepesi siyo kama hao wengine ni lazima uwaambie mapema." Mama Kadili alisema huku mkono mmoja akiwa ameshika kiuno.

"Kweli mama Gombea maana kuna watu wengine wazito, usipowaambia mapema imekuwa kwako."

"Enhee mwenzangu habari za mtaani umezisikia." Mama Gombea alipunguza sauti na haukuwa kama ile ya awali.

"Kwanza mwanao Kadili yupo?" Sauti huyo ilikuwa ya chini zaidi na kunong'oneza kuliko zote za mwanzo. "Mhh! Hayupo, ameniaga hapa anakwenda Kariakoo, sijui kaenda kununua nini?"

"Basi nasikia mwanao kampata msichana wa kitajiri."

"Unasemaje mama Gombea?" Ni kama vile hakusikia, au hakutarajia kuambiwa vile."

Hata hivyo Mama Kadili si mgeni kwa Mama Gombea, hakuna mtu yoyote Tandale ambaye hamfahamu mama huyo kwa tabia yake ya umbea. "Mwanao Kadili kama hajakwambia basi habari zikufikie mama mkwe, mwanao kapata msichana, lakini nasikia kwao matajiri sana."

"We mama Gombea, unataka kuniambia kuwa Kadili ana msichana wa kitajiri, mbona simuoni na lolote lile mwanangu hana mbele wala nyuma, si huyo binti kidogo angekuwa anamsaidia hata vinguo."

"Bado mambo hayajakaa sawa mama Kadili."

"Wewe umezipata wapi hizo habari?" "Bibi we unauliza makofi polisi, mimi ndiyo mama Gombea, na hilo trela tu, bado nitakujuza mengi. Ngoja niondoke mie nimuwahi mama Mtupeni, nisije kukutwa hapa nikasutwa." Alimaliza na kuondoka kwa madaha na kumuacha mwenyeji wake akimuangalia hadi alipokata kona.

Kwa mbali aliona kama maneno ya mama Gombea yana ukweli. Hata kama hawana ukweli kwa asilimia mia moja, lakini upo kwa asilimia 50.

Kwa muda wa wiki moja sasa kijana wake hayuko kwenye hali ya kawaida na hata jana yake alikaa naye kumuuliza swali hilo, lakini alikuwa akimpiga chenga na kumjibu hakuna chochote.

"Mtoto ana balaa huyu." Alijisemea mwenyewe. "Binti wa kitajiri sawa, lakini mbona kama ana mawazo mengi?" Alijiuliza na kuingia ndani kwenda kuipua chai yake.

**************************************

Mvua kubwa ilinyesha kwenye jiji la Dar es Salaam na kusababisha nyumba kujaa maji na shughuli nyingine kusimama, huku pia ikileta maafa.

Akiwa ndani kwake, mama Gombea alibandika sufuria yake ya ugali. Ni kawaida ya baadhi ya familia nyingi hasa uswahilini kutonunua unga na mchele na kuuweka ndani, badala yake wanapotaka kupika ndipo wanapokimbilia dukani kununua, kuanzia robo kilo na kuendelea kutosha kile ambacho wanakihitaji kwa mlo wa siku ile tu.

Aliamua kujitosa kwenye mvua kwenda kwenye duka la Meze kununua unga, nusu kilo kwa ajili ya chakula cha mchana yeye na familia yake. Alikuwa anakwenda hatua kwa hatua, nyumba kwa nyumba, kwa sababu ya mvua. Anatoka nyumba hii na kukimbilia nyuma nyingine anasimama.

Alifika kwenye dukani. Ndani ya duka kulikuwa na Meze pamoja na Kadili. Kutokana na tabia yake ya umbea, mama Gombea alisikia sauti na kutaka kujua nini kinaongelewa kabla ya kujitokeza dukani na kununua alichokihitaji.

Ndipo aliposikia mazungumzo ya vijana hao kuhusu msichana waliyekuwa naye kwenye hoteli ya 'Blue Star'. Na ndipo taarifa hiyo alipoipeleka kwa mama Kadili.

Hata hivyo ilikuwa ni taarifa ambayo haikukamilika kwa sababu hakuelewa vitu vingi kwa sababu hata Kadili na mwenzake Meze bado walikuwa hajajui vitu vingi kuhusu yule msichana.

Alichosikia ni vitu vichache tu.

"Mwanangu mimi nakwambia ukweli, yule msichana amekuzimikia."

"Wee Meze acha wee, siyo kweli sema yule mtoto kazimika jinsi nilivyokuwa nacheza tu."

"Hakuna yule mtoto wa kitajiri kakupenda, mimi nawajua mademu wa aina ile."

"Kusema kweli jinsi alivyo mwanangu, hata mimi nimempenda, ila yale maji marefu kwangu."

"Maji marefu gani Kadili wakati mtoto wa kishua kakupenda mwenyewe?"

***ITAENDELEA JUMAMOSI***

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.


***NIPASHE***
***NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0767 223311**


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**TWINS AUCTION MART CO. LTD & COURT BROKER** dalali wa Mahakama Mkoa wa Ruvuma kwa idhini tuliopewa na Mahakama kuu ya kanda ya Songea tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba kiwanja Na. 19 kitalu Na. "J" mali ya Changanyikeni SACCOSS iliyopo Manispaa ya Songea Wilaya ya Songea kesi Na. 6/2016&7/2016 na kesi na 3/2016 kati ya Robert Kunze na wenzake & TUICO Ruvuma dhidi ya Changanyikeni SACCOSS mnada utafanyika tarehe 5/7/2019 siku ya Ijumaa kuanzia saa 4:30 asubuhi.

**MASHARTI YA MNADA:**

Mnunuzi wa nyumba atakae bahatika atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa papo hapo na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo pesa iliyotolewa awali haitarudishwa na mnada utarudiwa tena. Gharama za kubadilisha hati **miliki (TRANSER OF OWNER SHIP)** ni za mteja mwenyewe na kiwanja kitaanza kukaguliwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:-**
**MKURUGENZI**
**S.L.P. 1305,**
**SONGEA.**
**SIMU NA. 0754881926; 0716070298; 0784 718734.**

115264802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 43..2019.**
**Mdai: NEEMA MANENO NASSORO**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: SALUMU SHARIFU HUSSEIN**

Kwa:
SALUMU SHARIFU HUSSEIN
WA SHINYANGA

Madai ya: **TARAKA, MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO.**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 17 mwezi 06 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 07 mwezi 06 mwaka 2019

115264802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;113/2019
Ombi la **GANJI MASHAKA SHABANI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ***MASHAKA SHABANI MOGELA***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 21/05/2019.

115264702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;122/2019

Ombi la **ELIZABETH GILLE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **JOHN SHITALILE GILLE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 4/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/06/2019.

115264602

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER SHILOGILE KITAMBI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T.181 CRN** aina ya TOYOTA LEXUS yenye engine namba Z852EX, Chasis namba **JTDBS182600069998,** Model namba **JTDBS1.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi: **GEI/MBO/RB/41711/2019.**

115263602

---

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
AT BUKOBA
CIVIL APPLICATION NO. 25/2018
ADOLFU GERVAS RWEYEMAMU...............APPLICANT
VERSUS
DENIS TRYPHONE KOMBA..................1ST RESPONDENT
NYANZA BOTTLING CO. LTD......2ND RESPONDENT

TO, ASTUTE LAW ATTORNEYS
KENYATA ROAD
PLOT NO. 12, BLOCK K,
NYANZA BUILDING, 3rd FLOOR
P.O. BOX 4026
MWANZA
TANZANIA

**RE: NOTICE OF DATE FOR HEARING**

Whereas the above Applicant lodged a case registered as Civil Application No. 25/2018 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said Case has been scheduled for mention on 3rd day of July, 2019 at 9:00 am before Hon. Judge L.G Kairo. You are authorized to appear in person or through your advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case may proceed in your absence.

Given under my hand and seal of this court this 3rd day of June 2019

115263802

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALOYCE SHIJA SHILINGI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T.805 CQF** aina ya CANTER yenye engine namba **4D33FE60095,** Chasisi namba **FE517BD500265.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

Taarifa ya Polisi:
**KAH /RB/ 490 /2019.**

115263902

---

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
AT BUKOBA
CIVIL APPLICATION NO. 25/2018
ADOLFU GERVAS RWEYEMAMU...............APPLICANT
VERSUS
DENIS TRYPHONE KOMBA..................1ST RESPONDENT
NYANZA BOTTLING CO. LTD......2ND RESPONDENT

TO, ASTUTE LAW ATTORNEYS
KENYATA ROAD
PLOT NO. 12, BLOCK K,
NYANZA BUILDING, 3rd FLOOR
P.O. BOX 4026
MWANZA, TANZANIA

**RE: NOTICE OF DATE FOR HEARING**

Whereas the above Applicant lodged a case registered as Civil Application No. 25/2018 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said Case has been scheduled for mention on 3rd day of July, 2019 at 9:00 am before Hon. Judge L.G Kairo. You are authorized to appear in person or through your advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case may proceed in your absence.

Given under my hand and seal of this court this 3rd day of June 2019

115264002

---

## CHETI KIMEPOTEA



**JULIUS LUGAZIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.115/0073 kilichotolewa na KAHORORO SEKONDARI BUKOBA mwaka 1980.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: CD/RB/3096/2019.

115264302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 66..2018.**
**Mdai: STEVEN FRANCIS MAKUNGA**
**DHIDI YA**

Mdaiwa: **SUZANA YASINDE MAKONDE**

**Kwa:**
**SUZANA YASINDE MAKONDE**
**WA MTAA WA MSIKITI-CHAMWINO.**
**Madai ya: TARAKA**

**Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo** juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 10 mwezi 06 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 27 mwezi 05 mwaka 2019

115264502

---

## KUPOTEA KWA KADI

**Sauli Anamkira Urassa** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **T 877 ACY,** gari aina ya **LAND CRUISER- TOYOTA,** Chasis namba **JTERB71J200011532.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa:**
**KW/K/B.I/VOL.291**

115263102

---

## KUPOTEA KWA KADI

**Josiah Mutahangarwa Munazi** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba T 230ABR gari aina ya NISSAN, Chasis namba JNITCSY61Z053130, Engine namba TD42162859.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa:**
**RB/6854/2019**

115262002


***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223 311***

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# CITY YAWEKA HADHARANI ITAKAOWASAJILI

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City imeshaweka wazi wachezaji inaowataka kwenye dirisha hili, Rodri, Harry Maguire na Aaron Wan-Bissaka huku ikifichua kutakuwa na panga litapita Etihad kusafisha wachezaji wasiohitahika.

Kocha Pep Guardiola anataka kuleta nyota wengine ili kuwa na njaa mpya ya mafanikio baada ya kubeba mataji matatu msimu uliopita, walipobeba Ligi Kuu England, Kombe la Ligi na Kombe la FA.

Nahodha wa City, Vincent Kompany ameshaondoka kwenye timu hiyo na imeelezwa kuna mastaa wengine kibao wa kikosi cha kwanza watafunguliwa mlango wa kutokea katika kikosi hicho.

Taarifa zilizopatikana zinasema kuwa City inataka kusajili kiungo wa kati, beki wa kati na beki wa kulia katika dirisha hili la majira ya kiangazi huko Ulaya.

Kwa sababu Fernandinho umri umeshaanza kumtupa mkono akiwa na miaka 34 kwa sasa, City sasa inampigia hesabu staa wa Atletico Madrid, Rodri ikitaka akachukue nafasi huko Etihad na imeshakubali kulipa pauni milioni 62 zilizobainishwa kwenye mkataba wa mchezaji huyo.

Staa mwingine wanayemsaka ni kiungo wa Lyon, Tanguy Ndombele na wa Real Madrid, Marcos Llorente.





# UNITED YAMWANIA MRITHI WA LUKAKU

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa timu ya Frankfurt, Sebastien Haller kwa ajili ya msimu ujao.

United wanaitaka saini ya mchezaji huyo ili awe mbadala wa nyota wao, Romelu Lukaku ambaye anahitaji kuondoka ndani ya kikosi hicho.

Kikosi cha Inter Milan ya Italia kimeonyesha nia ya kupata saini ya mchezaji huyo ambaye ni mshambuliaji anayekipiga pia katika Timu ya Taifa ya Ubelgiji.

Mabosi wa United wapo tayari kumuuza Lukaku kwa dau la Euro milioni 80 kwa kuwa wanajua kwamba Lukaku ni chaguo la Antonie Conte ambaye inasemekana atakuwa meneja wa kikosi hicho.

Wafuatiliaji wa wachezaji kutoka United wamesema kuwa Haller atakuwa ni mbadala wa Lukaku kutokana na uwezo wake wa kutupia mabao ambapo kwenye ligi ya Bundesliga amefunga jumla ya magoli 15 kwenye mechi zake 23 za mwanzo.

# Dortmund yaibania Arsenal kumnasa Gotze

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, anaelekea kukwama kwenye mpango wake wa kumnasa Mario Gotze baada ya Borussia Dortmund kudai ipo kwenye mazungumzo ya kumwongezea mkataba mpya, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani.

Mkataba wa sasa wa Gotze pale Dortmund unafika tamati mwakani, lakini mabosi wa timu hiyo wanataka kumpa dili jipya ili kumtibulia Emery ambaye alikuwa akiamini angemnasa staa huyo na kumleta kwenye Ligi Kuu England.

Emery alikuwa akipiga hesabu za kumnasa Gotze, kwa sababu anafahamu wazi atampata kwa dili la chini kidogo, huku msimu uliomalizika hivi karibuni huko kwenye Bundesliga alionyesha kuwa fiti na hakusumbuliwa na majeruhi.

Mkurugenzi wa michezo wa Dortmund, Michael Zorc, alisema mpango wa timu hiyo ni kumbakiza Gotze kwenye kikosi chao, alisema: "Tumesikia tetesi nyingi za kutoka England kwa miaka mingi. Lakini, kama kawaida yetu, siku zote tumekuwa hatuna wasiwasi.

"Gotze hajatufuata kuomba kuhama. Na kwa sasa tumekuwa kwenye mazungumzo mazuri na baba na wakala wake. Mwanzo wa msimu ujao, tutaketi na kuzungumza kuhusu mkataba mpya."


Arsenal imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumsajili Gotze tangu mwaka 2011 kipindi hicho alipoibukia kwenye soka akiwa kinda mdogo na kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger alisema wakati ule: "Gotze ni mchezeshaji, ni mmoja kati ya wachezaji wazuri kwa asisti Ujerumani na pia ni mchezaji hatari."



## HABARI MICHEZO

# SOUTHGATE

## AJITETEA ENGLAND IKICHAPWA



**AMSTERDAM, Uholanzi**

KOCHA wa England, Gareth Southgate, aliachwa na mshituko baada ya safu yake ya ulinzi kufanya makosa kwenye muda wa ziada na kuwazawadia Uholanzi ushindi wa mabao 3-1 katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la Ligi ya Mataifa ya Ulaya.

Hata hivyo, hakuwa tayari kuwalaumu wachezaji wake kwani walipigana vya kutosha kutafuta ushindi.

Makosa ya John Stones yakaifanya Uholanzi kuwa mbele kwa mabao 2-1 na baadaye pasi fupi ya Ross Barkley ikaifanya England kuambulia kipigo hicho.

"Kuchoka ilikuwa sababu ya wachezaji wangu kucheza kwa makosa usiku wa leo (juzi)," alisema Southgate mara baada ya mchezo huo.

"Nilliwaomba wacheze kwa kujituma kwa sababu mchezo uliokuwa mgumu, lakini tulishindwa kupata matokeo licha ya kuanza kwa kuongoza," alisema.

"Uholanzi pia ilifanya makosa makubwa hasa wakati Matthijs de Ligt aliposababisha penalti iliyotupa bao la uongozi.

"Tumefungwa sio kwa sababu tulitaka kucheza vile, hapana, tumefungwa kutokana na kuchoka kwa wachezaji wetu."

Kipigo hicho kinamaanisha kwamba wamefungwa tena kwenye nusu fainali katika mashindano makubwa baada ya kufika hatua hiyo katika michuano ya Kombe la Dunia mwaka 1990 na 2018 pamoja na lile la Mataifa ya Ulaya ya mwaka 1996.

"Tulizungumza kabla ya mchezo kwamba tunahitaji kupita mafanikio tuliyoyapata kwenye michuano iliyopita.

"Lakini makosa yetu yametufanya tushindwe kufikia malengo tuliyoyaweka na kwa uhakika tulikuwa na nafasi ya kupata ushindi kwenye mchezo ule," aliongeza kusema Southgate.

Mshambuliaji kijana wa Manchester United, Marcus Rashford, alianza kwa kuipatia bao la uongozi England kwa mkwaju wa penalti.

Lakini penalti hiyo haikutosha kuwahakikishia ushindi England na kujikuta wakiadhibiwa na wadachi hao.



## Mwanamke 'aliyebakwa' na Neymar ajitokeza

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

MWANAMKE aliyedai kubakwa na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Neymar, amejitokeza hadharani na kumshutumu mchezaji huyo katika runinga moja ya nchini humo.

Mwanamke huyo anayeitwa Najila Trindade aliambia runinga ya SBT nchini Brazil kwamba kisa hicho kilichotokea katika hoteli moja ya Paris Mei 15 mwaka huu kilikuwa cha unyanyasaji pamoja na ubakaji.

Neymar amekana madai hayo, akituma ujumbe wa whats App ili kujaribu kuonyesha kwamba hana hatia.

Aliichezea kwa muda mfupi timu yake ya Brazil siku ya Jumatano katika mechi aliyodai kuwa ngumu katika kipindi chote cha uchezaji wake.

Neymar alipata jeraha baada ya dakika 20 ya mechi hiyo dhidi ya Qatar mjini Brasilia na sasa atakosa kushiriki katika michuano ya Kombe la Copa America 2019 nchini Brazil akiwa na jeraha la mguu.

Trindade anasema kuwa alivutiwa na mchezaji huyo wa PSG na Brazil na alitaka kushiriki ngono naye.

Anasema alisafarishwa kwa ndege hadi mjini Paris na kulipiwa katika hoteli moja ya jijini Paris.

Aliyekuwa akimhoji alimuuliza Trindade iwapo kile kilichotokea ulikuwa ubakaji na alijibu kwamba ulikuwa unyanyasaji wa kingono na ubakaji.

Amesema kwamba wakati walipokutana na Neymar alikuwa mtu wa fujo na mtu tofauti na yule aliyemjua katika ujumbe.

## Mpango wa Pogba kurudi Juventus waiva



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Juventus imeonyesha nia ya kutaka kumsajili tena kiungo wa klabu ya Manchester United, Paul Pogba kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake katika msimu ujao wa Ligi Kuu Italia na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Juventus Mabingwa wa Ligi Kuu Italia imewasiliana na wakala wa mchezaji huyo Mino Raiola juu ya kutaka huduma ya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26 ambaye ni raia wa Ufaransa.

Ikumbukwe kuwa kwa mara ya kwanza Pogba alijiunga na Juventus kwa uhamisho huru mwaka 2012, baada ya kushindwa kupata nafasi katika kikosi cha kwanza klabu ya mpira ya Old Trafford.

Hata hivyo, mchezaji huyo nyota aliyeitumikia Juventus miaka minne kwa mafanikio makubwa kabla ya kujiunga tena na United mwaka 2016 kwa kitita cha pauni milioni 89 kiasi ambacho kilivunja rekodi ya Dunia.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ACHAGUA KUTUA BARCELONA

●●● Hata hivyo PSG wafunguka hawajaonyesha nia yoyote ya kutaka kumuuza...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI Mbrazil, Neymar ameiambia wazi klabu ya Paris Saint-Germain kuwa anataka kujiunga na Barcelona tu na si klabu nyingine licha ya Real Madrid kuonyesha nia ya kutaka nyota huyo akaitumikie klabu hiyo ya Bernabeu.

Mbrazil huyo ambaye ameitumikia kwa misimu miwili klabu hiyo ya jijini Paris, amekuwa hana furaha kwa muda mrefu licha ya kuonekana kutakiwa na vigogo hao katika kipindi cha majira ya joto.

Madrid imeonyesha kuweka nguvu zaidi katika mchakato huo, lakini taarifa zinasema kuwa Neymar ameamua kukacha ofa hiyo.

Gazeti moja la Hispania limeandika kuwa, Rais wa Madrid, Florentino Perez na Makamu wake, Jose Angel Sanchez kwa pamoja wamejaribu kumshawishi kwa namna mbalimbali mshambuliaji huyo atue Bernabeu lakini nyota huyo ameweka wazi kwamba anataka kurejea katika klabu yake ya zamani kama atafikia uamuzi wa kuondoka.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alijiunga na PSG mwaka 2017 akitokea Barca kwa dau la pauni milioni 198 ambalo liliweka rekodi ya usajili duniani, amefunga mabao 68 katika mechi 123 alizocheza kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.

Klabu hiyo ya Ufaransa haina nia yoyote ya kutaka kumuuza mchezaji huyo kwa sababu inataka aendelee kuwa sehemu ya kikosi kitakachopambana kuhakikisha wanashinda taji la Ligi la Mabingwa Ulaya.

Neymar amefuta ndoto za kuisaidia timu yake kuwania Kombe la Copa America kutokana na kuwa majeruhi baada ya kuumia katika mechi ya kirafiki dhidi ya Qatar.

Alipata maumivu hayo dakika ya 20 ya mechi hiyo ambayo kikosi chao maarufu Selecao kiliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Qatar, katika mchezo uliochezwa Jumatano iliyopita na kutolewa nje na jopo la madaktari wa Brazil. Alionekana akiwa na uchungu na kuanza kulia kutokana na changamoto hiyo aliyopata.

Nahodha huyo wa zamani alionekana kukaa chini katika dakika za mapema za mchezo huo baada ya kuhisi maumivu, na kutokana na hali hiyo, madaktari walimfuata na kuangalia tatizo lake.

Neymar aliondolewa uwanjani haraka akiwa amewekewa kipande kikubwa cha barafu na kuwahishwa kwenye Uwanja wa Ndege ili akapatiwe matibabu zaidi ya enka ambayo yalimpata.

## KWA UFUPI

### CANCELO ANUKIA CITY
BEKI wa kulia wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Cancelo (25), huenda akajiunga na Manchester City kwa dau la pauni milioni 44, kama The Blues watamuuza nyota Mbrazil Danilo ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Goal)***

### DRAXLER KUMRITHI ERIKSEN
KLABU ya Tottenham imewasilisha ofa ya kumwania mshambuliaji wa PSG Mjerumani Julian Draxler (25), ili kuziba nafasi ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), kama nyota huyo ataamua kuondoka katika klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Star)***

### EVERTON, SPURS WATETA
EVERTON imewasiliana na Spurs na kuwaeleza kuwa wanataka kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya England, Danny Rose kama itafikia makubaliano ya kumruhusu beki wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Lucas Digne (25), kuondoka Goodison Park. ***(Star)***

### UNITED YAJITOA
MANCHESTER United imejiondoa katika mbio za kumwania beki wa Ajax, Matthijs de Ligt, baada ya Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 19 kuonyesha kuchagua kujiunga ama na klabu ya Paris St-Germain au Barcelona. ***(Marca)***

### DE LIGT AKARIBIA PSG
MABINGWA wa Ligi Kuu Ufaransa Paris St-Germain inapewa nafasi kubwa ya kumsajili beki wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Mayyhijs de Ligt katika kipindi cha majira ya joto. ***(ESPN)***

### UNITED KUFANYA KWELI
MABOSI wa Manchester United, wamesema kuwa watasajili wachezaji wawili wapya ambao ni bora ndani ya mwezi huu, kabla ya kikosi chao hakijaanza maandalizi ya msimu mpya. ***(Sun)***

### TIELEMANS KUMRITHI POGBA
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji na Monaco, Youri Tielemans (22), ambaye msimu uliomalizika aliitumikia Leicester City kwa mkopo, anatakiwa na United kama kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba (26) ataondoka Old Trafford katika kipindi cha majira ya joto. ***(Independent)***

### MAGUIRE ANUKIA CITY
BEKI wa Leicester na Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire (26), anajiandaa kukacha ofa ya kujiunga na Manchester United, na kueleza kwamba anataka kuelekea Manchester City. ***(Mail)***

### MADDISON ATOA MSIMAMO
KIUNGO wa Leicester maarufu The Foxes, James Maddison, amesema anataka kubakia King Power licha ya kuwapo na tetesi za mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya England kutakiwa na Manchester United na Tottenham. ***(Mail)***

### GUEYE ATAKIWA PSG
MABOSI wa Paris St-Germain wanatarajia kurejea kwa mara nyingine katika klabu ya Everton kuwasilisha ofa ya kumwania kiungo, Idrissa Gueye (29), katika kipindi cha majira ya joto. ***(Le 10 Sport - in French)***

### ARSENAL KUMNASA CARRASCO
WINGA wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Yannick Carrasco (25), anakaribia kukamilisha mchakato wa kujiunga na Arsenal akitokea katika klabu ya Dalian Yifang ambayo inashiriki Ligi Kuu China. ***(Mirror)***

### DARMIAN ATAKIWA VALENCIA
VALENCIA imeweka wazi kuwa iko tayari kutoa pauni milioni nane kwa Manchester United ili kumnasa beki wa Timu ya Taifa ya Italia, Matteo Darmian ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Mail)***



# KAGERA SUGAR, MWADUI NI KUFA NA KUPONA LEO

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMA ya timu zinazowania nafasi ya kubakia au kupanda daraja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kufahamika baada ya kumalizika kwa mechi za marudiano za Play Off zitakazochezwa leo kwenye viwanja viwili tofauti nchini.

Mechi ya kwanza itakuwa kati ya Kagera Sugar dhidi ya Pamba FC ambayo itachezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba Mjini Bukoba na nyingine itawakutanisha Mwadui FC dhidi ya Geita Gold FC kwenye Uwanja wa Mwadui Complex mkoani Shinyanga.

Katika mechi za kwanza zilizochezwa wiki iliyopita, matokeo yalikuwa ni sare ya bila kufungana na inamaanisha kuwa timu zitakazopata ushindi leo, zitakuwa zimekata tiketi ya kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2019/20.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, aliliambia gazeti hili kwamba wamejiandaa kupambana katika mechi ya leo ili wapate ushindi na hatimaye kubakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu mwingine zaidi.

Maxime alisema mechi hiyo ya marudiano haitakuwa nyepesi, kwa sababu kila timu ina nafasi sawa na lolote linaweza kutokea katika mchezo wa soka.

"Inaitwa hakuna kulala, ukizembea unapigwa na unashuka daraja, kwa mapenzi ya Mungu, naamini tutafanya kila ambacho tunakitarajia," alisema kocha huyo.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Soka Geita, Pius Kimisha, alisema kuwa wachezaji wote wa Geita Gold wako katika hali nzuri na wanachoomba ni kuona wanajituma na hatimaye kupata ushindi katika mchezo wa leo.

"Tunatarajia na tulijua mapema kuwa mechi za Play Off ni ngumu, ila nafasi ya kutimiza ndoto zetu kwa kupanda daraja bado zipo, tunaomba ushirikiano tulioupata kutoka kwa wadau wetu uendelee," alisema Kimisha.

Tayari Namungo FC na Polisi Tanzania zimeshapanda daraja wakati zilizoteremka hadi Ligi Daraja la Kwanza ni African Lyon ya Dar es Salaam na Stand United ya Shinyanga.



Baadhi ya wachezaji wa zamani Timu ya Taifa (Taifa Stars) ambao walishiriki katika Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 1980), wakiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Dk. Yusuf Singo (wa pili kulia) pamoja na maofisa wa Kampuni ya Multihoice Tanzania katika uzinduzi wa kampeni ya 'DSTV Tupogo' jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Namungo yatajwa kuivuruga Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

ILI kukabiliana na ushindani katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2019/20, uongozi wa Namungo FC ya Lindi, unatajwa kuwa kwenye mazungumzo ya kumsajili kipa wa Yanga, Ramadhani Kabwili, imeelezwa.

Tayari Namungo FC imefanikiwa kumsajili mshambuliaji wa Alliance FC, Bigirimana Blaise kwa kumpa mkataba wa mwaka mmoja.

Taarifa kutoka jijini Dar es Salaam zinaeleza kuwa tayari Namungo na Kabwili wameanza mazungumzo na golikipa huyo wa zamani wa Serengeti Boys na endapo yatakamilika, atasaini mkataba na timu hiyo iliyopanda daraja msimu huu ili aongeze nguvu katika kikosi chao.

Habari kutoka Yanga zinasema kuwa kwa sasa Kabwili ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake wa awali wa miaka miwili na timu hiyo iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera.

"Sisi tunajipanga kujiimarisha, na taarifa rasmi tulizonazo ni kuwa Kabwili ni mchezaji huru baada ya mkataba wake na Yanga kumalizika, huku hakuna kiongozi aliyemwita kukaa mezani kuzungumzia usajili wake," alisema kiongozi mmoja wa Namungo.

Ofisa Habari wa Namungo, Kidamba Namlia, alisema kuwa klabu yao imejipanga kusajili wachezaji wenye uwezo na uzoefu ambao utawasaidia kufanya vema katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Ligi Kuu inaushindani sana, ili tuweze kuimudu ni lazima tusajili wachezaji wenye nguvu na watakaotupa matokeo mazuri, hatutaki kuona tunasindikiza wengine, tumejiandaa kuja kushindana," Namlia alisema.

Klabu hiyp pia imewaongezea mkataba wachezaji wake wengine watatu ambao ni pamoja na Jukumu Kibanda, Lusajo Reliants na Daniel Joram.

## Dstv kuisogeza Afcon nyumbani

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku chache kabla ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2019) kuanza huko nchini Misri, Kampuni ya MultiChoice Tanzania (DStv) imetangaza rasmi kampeni maalumu kwa Watanzania itakayowawezesha kushuhudia michezo yote 52 ya michuano hiyo kupitia chaneli za Supersport zilizo katika mfumo wa HD.

Akizungumza katika hafla ya kuzindua kampeni hiyo ya DStv ijulikanayo kama 'DStv Tupogo', Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, alisema kuwa kampuni yao inafuraha kuwapatia burudani hiyo mashabiki wa soka wa hapa nchini ambao wataiona timu yao ya Taifa (Taifa Stars) ambayo itashiriki fainali hizo.

"Tuna furaha kubwa kwa nchi yetu kupata fursa ya kushiriki katika michuano hii ya kimataifa baada ya takribani miaka 39 tangu iliposhiriki kwa mara ya mwisho mwaka 1980. Na kama ilivyo ada, ni jukumu letu na la kila Mtanzania kuhakikisha kuwa tunawatia moyo vijana wetu na kuifanya nchi yetu ifanye vizuri katika michuano hii ya kimataifa.

Kwa kuzingatia hilo, DStv imehakikisha kuwa mechi zote za michuano hii ya kimataifa zitarushwa mubashara DStv kupitia chaneli za Supersport na kwa lugha adhimu ya Kiswahili, Dstv imehakikisha kuwa mechi hizo zinaonekana katika vifurushi vyote kuanzia kile cha chini kiitwacho DStv Bomba ambacho gharama yake ni Sh. 19,000 tu. "Tumehakikisha kuwa mechi hizi zinakuwepo hadi kwenye kifurushi cha chini kabisa ili kuwawezesha Watanzania wengi kushuhudia mtanange huo na kuwa sehemu ya historia ya nchi yetu kwani tunashiriki baada ya zaidi ya miaka 30", alisema Woiso.

Alisema kuwa mechi hizo zitatangazwa kwa lugha ya kiswahili kwa kutumia watangazaji maarufu wa hapa nchini huku pia wakimtambulisha mchambuzi mpya mwanamke ambaye ni Salama Jabir atakayeungana na wakongwe, Aboubakar Liongo, Ibrahim Maestro, Edo Kumwembe, Maulid Kitenge na Oscar Oscar.


Naye Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo alisema, "Wateja wa DStv pia wataweza kupokea matangazo ya moja kwa moja kwa kupitia application ya "DStv Now" kupitia katika vifaa mbalimbali ikiwamo simu ya mkononi, lap top au tablet na televisheni ya kawaida".

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Dk. Yusuph Singo alisema kuwa kitendo cha DStv kuonyesha mubashara michuano hiyo ni cha kupongezwa kwani ni sifa kubwa kwa nchi yetu. Singo alisema kuwa mchango mkubwa unaotolewa na MultiChoice Tanzania katika sekta ya michezo umechangia sana katika kukuza michezo na kuliletea taifa sifa kubwa.

# Michezo

Jumamosi Juni 8, 2019

Nipashe

Neymar achagua kutua Barcelona

HABARI UK 30

# AJIBU, MKUDE WAACHWA STARS

●●●Wadau watofautiana na uamuzi huo uliofanywa na Amunike kuelekea Afcon...

**Na Somoe Ng'itu**

NAHODHA na mshambuliaji wa Yanga, Ibrahim Ajibu na kiungo wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Jonas Mkude ni kati ya wachezaji waliotemwa katika mchujo wa awali wa kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars) ambacho kiliondoka nchini jana kuelekea Misri kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), imefahamika.

Nyota wengine wa timu hiyo walioachwa katika kikosi hicho na Kocha Mkuu Mnigeria Emmanuel Amunike ni pamoja na beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, Kennedy Wilson ( Singida United, Ally Ally (KMC), Khamis Khamis (Kagera Sugar) na Ayoub Lyanga wa Coastal Union ya jijini Tanga.

Mchujo wa pili wa wachezaji wa timu hiyo iliyoko Kundi C katika michuano hiyo utafanywa huko Misri kwa kubakiza nyota 23 ambao ndio watapeperusha bendera ya Tanzania kwenye fainali hizo zinazotarajiwa kuchezwa kuanzia Juni 21 hadi Julai 19 mwaka huu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Amunike, alisema kuwa amewaacha wachezaji hao kutokana na kuonyesha kiwango cha chini mazoezini na vile vile kukosa nidhamu.

Amunike alisema ili mchezaji uweze kuwa katika kikosi chake ni lazima uwe unajituma na kumshawishi bila ya kuangalia mchezaji anatoka kwenye timu gani ndani au nje ya nchi.

"Kwangu siangalii umetoka wapi, naangalia utaisaidia nini timu, tulianza safari hii tukiwa na wachezaji wengi, wengine hawapo hapa, Tumemwacha Ajibu, tumemwacha Mkude, Khamisi, Ayoub, Kennedy, tunajua kuwa Kapombe ni mgonjwa, hawa ni wachezaji ambao hatutaenda nao Cairo," alisema Amunike.

Kocha huyo aliongeza kuwa yeye pia ni Mwafrika na kama hatakuwa mkweli katika kuzingatia vigezo vyake katika kuinua maendeleo ya mchezo huo hapa nchini, Tanzania haitaweza kusonga mbele na anaamini huo msimamo wake.

"Uteuzi huu hausiani na kiwango tu, nataka kuwa mkweli, kutenda haki, kama huwezi kufanya mazoezi, huna nidhamu, huwezi kusonga mbele...hata mimi nisingekuwa na nidhamu nisingecheza Barcelona," alisisitiza kocha huyo ambaye anasaidiwa na Mzanzibar Hemed Morocco.

Aliongeza kuwa soka si kama hesabu, unatakiwa kuzingatia misingi ya programu za timu na hapo timu itakuwa na nafasi ya kufanya vema.



Nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta (kulia), akimfunga tai mshambuliaji mwenzake wa timu hiyo, Thomas Ulimwengu, muda mchache kabla ya kupanda ndege kuelekea Misri. **PICHA: MTANDAO**

"Nataka wachezaji wazuri ambao watakwenda kupeperusha bendera ya nchi, tukijituma tutapata matokeo mazuri, Tunaenda kushinda, tunaenda kupoteza, hakuna anayejua, timu 24 zitashiriki mashindano hayo, kila mmoja anaamini atafanya vizuri, lakini kwa faida ya baadaye, Tanzania itaendelea kuimarika," aliongeza.

Amani Rweikiza aliliambia gazeti hili kuwa Mkude ni mmoja wa viungo wakabaji mahiri nchini, na kuachwa kwake kumemshangaza.

"Kwa Ajibu kweli nidhamu yake inaweza kuwa na mashaka kidogo, kwa Mkude hakuna upinzani kuwa ni kiungo mkabaji mzuri sana pengine kuliko yoyote katika hao waliobaki ila tu nafikiri nyota yake na Amunike hazipikiki chungu kimoja," alisema mdau huyo.

Mdau mwingine, alisema kuwa hakubaliani na uamuzi wa kocha huyo ambaye baada ya kumalizika kwa fainali za Afcon, atakuwa na jukumu lingine la mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani maarufu CHAN.

"Baada ya Afcon tuna mashindano ya CHAN, sasa nikisoma majina ya washambuliaji namuona Bocco (John) peke yake, ni shida kidogo," alisema mdau huyo ambaye ni daktari bingwa hapa nchini (jina tunalihifadhi).

Mecky Maxime, nahodha na beki wa zamani wa Stars alisema kuwa hatarajii kuona timu hiyo inafanya vema katika michuano hiyo kutokana na maamuzi mbalimbali yanayofanywa na kocha huyo ambaye amepata bahati ya kuipeleka Tanzania katika fainali hizo.

Kikosi kilichoondoka jana kinajumuisha makipa watano ambao ni Aishi Manula (Simba SC), Metacha Mnata (Mbao), Aron Kalambo (Tz Prisons), Selemani Salula (Malindi) na Claryo Boniface (U20) huku mabeki wakiwa ni Hassan Kessy (Nkana, Zambia), Vicent Philipo (Mbao), Gadiel Michael (Yanga), Mohamed Hussein, Erasto Nyoni (Simba), Ally Sonso (Lipuli), Kelvin Yondani (Yanga), David Mwantika (Azam), Agrey Moris (Azam) na Abdi Banda kutoka Baroka ya Afrika Kusini.

Viungo ni Mudathir Yahya, Frank Domayo (Azam), Feisal Salum (Yanga), Fred Tangalu (Lipuli) wakati Saimon Msuva (Difaa El Jadid), Shiza Kichuya (ENPPI), Farid Mussa (Tenerife), Miraji Athumani (Lipuli), Yahya Zayd (Ismaily) na -Himid Mao wa Petrojet atakayeungana na timu hiyo huko huko Misri ndio mawinga na washambuliaji ni Thomas Ulimwengu (JS Soura), Shabani Chulunda (Tenerife), Bocco (Simba), Mbwana Samatta (Genk), Kelvin John Mbappé (U17), Rashid Mandawa (BDF) na Adi Yussuf wa Solihull Moors ya England.

## Kagere aendelea kung'ara Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam umesema kuwa unajipanga kuhakikisha timu yao inaweka kambi katika mahali bora zaidi, mshambuliaji wake, Meddie Kagere ametajwa kuwa Mchezaji Bora wa ligi hiyo mwezi Mei.

**Kagere ambaye pia ni Mfungaji Bora wa ligi hiyo ya msimu wa 2018/19 iliyomalizika hivi karibuni, ameshinda tuzo hiyo baada ya kuwazidi kura mshambuliaji mpya wa Namungo, Bigirimana Blaise aliyekuwa Alliance na Tariq Kiakala wa Biashara United ya Musoma mkoani Mara.**

Mnyarwanda huyo ambaye hiyo ni tuzo yake ya pili katika tuzo hizo, wiki iliyopita alitangazwa pia kuwa Mchezaji Bora wa Mwaka wa Simba katika tuzo zilizotolewa na klabu yake.

Kamati ya Tuzo pia jana ilimtangaza Kocha Mkuu wa KMC, Ettiene Ndayiragije kuwa mshindi wa tuzo ya Kocha Bora wa mwezi uliopita ambao ndio ligi ilifika tamati.

Ndayiragije ameiongoza KMC kumaliza katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo baada ya kujikusanyia pointi 52 na kuwashinda Patrick Aussems wa Simba na Malale Hamsini wa Alliance FC ya jijini Mwanza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili kuwa wanatarajia kuwa na kambi ya wiki sita huko ughaibuni na ndio maana wamefikia uamuzi wa kujitoa kushiriki mashindano ya Kombe la Kagame ili kujiandaa vema kwa sababu wanataka kufanya vizuri zaidi katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >